# CONSTITUTION OF KENYA REVIEW COMMISSION

# (CKRC)

## Verbatim Report Of

## DISSEMINATION OF REPORT AND DRAFTS BILL CHERENGANI CONSTITUENCY. KACHIBORA FRIENDS CHURCH HALL

ON

**11th OCTOBER 2002**

**CONSTITUTION OF KENYA REVIEW COMMISSION**

**DISSEMINATION OF REPORT AND DRAFTS BILL, CHERANGANI CONSTITUENCY, HELD AT KACHIBORA FRIENDS CHURCH ON 7TH OCTOBER 2002**

**Present**

Com. Salome Muigai

**Secretariat in Attendance**

Dan Juma – Assistant Programme Officer
Asenath Kanga - Verbatim Recorder.
Emmanuel Satia - District Coordinator.

**The Meeting started at 11.45 am with Com. Salome Muigai in Chair**

**Pastor John Wachie:** Tuondoe kofia ili tuombe. Baba katika jina la Yesu Kristo, tunakuja mbele yako kwa wakati huu, ambapo tumekusanyika mahali hapa, ni kwa ajili ya mkutano wa siku ya leo, kuangalia mambo ya Katiba, Mungu tunakuomba ya kwamba tunapoanza mazungumzo, ukaweze kuwa pamoja nasi, ukaweze kutuongoza, ukaweze kutusaidia, hata tutakapo maliza huu mkutano, tumalize ukiwa pamoja nawe. Baba tunakushuru kwa ajili ya afya, tunakushukuru kwa ajili ya uzima, tunakushukuru kutuwesesha tuwe wazima ili tuwe mahali hapa, kwa sababu bila wewe hatungeweza kukusanyika njizi tulivyo. Tunakumbuka nchi yetu ya Kenya, tunakumbuka Serikali yetu, Bwana hasa wakati huu mgumu ambao uchumi umefilisika, wakati mbao ni mgumu tunashughulika na mambo ya kura, waalimu wako katika mgomo, Mungu tunaomba ukaweze kuleta maelewano mazuri kati ya walimu na Serikali ili Bwana watoto wakaweze kurudi shule, na kuendelea na mitihani yao. Bwana tunakushuru kwa kila mmoja ya kwamba utaleta amani katika nchi yetu ya Kenya tunapo pitia katika hali ngumu hii. Ukaweze kutuongoza na kutusaidia na haza kutupa njia ili hii nchi ikaweze kuendelea mbele. Kutusaidia na zaidi wakutambue na kukutumikia kupitia mikononi mwao. Ninakushukuru na ninakuinua kwa sababu utakuwa pamoja nasi mahali hapa na ni kwa jina la Yesu Kristo nimeomba nikiamini. Amina. Mungu awabariki

**Audience**: Amina..

**Emmanuel Satia**: Asante sana kwa maombi, kwanza kabisa, kabla ya kusema chochote, ningelipenda kwanza kuomba msamaha kwa sababu tumekuja tukiwa tumechelewa na tulitarajia tuje leo. Lakini ilibidi tupitie katika ofisi ya mkuu wa wilaya na katika ofisi ya mkubwa hauwezi kuwa na haraka. Siju kama mtatusamee.?

**Audince**: Tutawasemea.

**Emmanuel Satia**: Asante sana.. Haya pili, ningalipenda kuchukua nafasi hii kwanza kabisa kuwashukuru kwa sababu ya kuja kwenu kwa wingi wakati wa kutoa maoni kwa Tume, na pia leo kwa sababu ya kupata nafasi ya kuja kushiriki nasi ilituweze kuangalia Katiba hii mpya inayo pendegezwa inasema nini.

Na kabla ya kuanza mkutano, ningelipenda kuchukua nafasi hii kuwajulisheni wale wana kamati ambao tumekuwa tukifanya kazi noa pamoja katika wilaya hii yetu ya Trans Nzioa. Tuna wana kamati ambao wameketi hapa mbele upande wa kulia labda nitwauliza wasimame ninapowataja majina ili kila mtu apate kuona ni akina nani.

Kule mwisho kabisa kuna Gerald Ndege ambaye ni mwana kamati kutoka katika eneo la Kwanza, anafuata na Bwana John Kibet ambaye ni pia anatoka upande wa kwanza, Bi Veronicah Kibet ni wa hapa hapa. Chepketeri Edah, pia ni mwana kamati na pia kutoka sehemu hii, Mrs. Nancy Iyaki ni mwana kamati kutoka upande wa Saboti lakini pia ndiye mama atakaye waakilisha akina mama katika kikao hicho cha National Conference kule Nairobi. Kisha kuna Busara Kombo, yeye pia anatoka Cherengani ambaye pia ataenda Nairobi anayefuatia ni mama Bi. Julia Victor ambaye ni mwakilishi wa Saboti. Na mwisho kabisha ninajua mtasema mnamfahamu, lakini waja nimjulishe, anaitwa Joseph Chebii ambaye ni mwana kamati anaketi katika ile kamati kwa niaba ya Mheshimiwa Ziporah Kitonyi. Halafu na upande wetu wa kushoto ni Bi. Mary Nyambane ambaye ni mwakilishi kutoka upande wa Saboti.

Commissioner ningalipenda kuchukua nafasi hii, nikuombe uweze kuwajulisha wananchi wale ma-officer ambao umekuja nao kisha utuelekeze. Mimi ni co-ordinator, naitwa Emmanuel Satia. Karibuni.

**Com. Salome Muigai:** Mabibi na Mabwana ninataka kuwajulisha wale tumekuja nao kutoka kutoka Nairobi na kabla sijanza, tunawaomba msamaha kwa kuja kama tumejechelewa kama vile bwana coordinator alivyo sema tumepitia kwa Bwana DC ili atupe ufunguo wa kukaa kwa wilaya yake. Hatungekaa kwa wilaya yake pia kumuuliza kwa hivyo leo, tutaanza kikao chetu cha mwisho kuwa hapa kwenye wilaya yenu ya Transnzoia, tuombe tutafanya kazi bila kuchoka nasikia tutawasiliana nanyi huko Bomas of Kenya wakati wa Conference.

Nimekuja na ma-officer, watatu kutoka ofisini kwetu, pale mbele kuna Bwana David Kamau, naodha wetu, pia kuna Bi. Asanath Kanga ndiye atakuwa akifanya tapping ya kuchukua notes za huu mkutano na kwa upande wangu wa kushoto tuna Bwana Juma ambaye ni Asssistant Programe Officer kutoka kwenye ofisi yetu ya Nairobi, na mimi mwenyewe jina langu ni

Com. Salome Wairimu Muigai na ninashukuru kwa kuja hapa.

Kazi yetu leo ni kazi rahisi ya kurudisha na kuwaelezea Katiba yenye tumetoa kwa yale maoni yenye mlitupatia. Kazi yetu ya kwanza ilikuwa kuja hapa na kusikiliza maoni yenu, halafu tukafanya kazi ya kuyachukua maoni na kuyaangalia na kuaangalia ile maneno yenye mlikuawa mmentwambia na kutengeneza ama kuaandika report. Kwa hivyo tuliandika report mbili. Ya kwanza ni report tunayoita Short Version, the People's Choice, ni maoni ya Kenya nzima lakini kwa ufupi. Tumeiandika pia kwa Kiswahili, Chakuao la Watu, sijui kama mliiona kwa magazeti karibu mwezi mmoja uliopita hivi, mliona?

**Audience**: Tuliona.

**Com. Salome Muigai**: Tumeona kila mtu ameiona. Halafu tumekuja na hii report, tumeweza kuteng'eneza msuada wa kugeuza Katiba yetu. Na leo siku ya leo ni kuangalia huo mswada, kuangalia kama umeleta matakwa yenu na maoni yenu na kuyatia maanani na kubadilisha ikawa sheria. Itakuwa sheria, wakati itapelekwa kwa mkutano wa kikao cha Taifa chenye kitakachoendelea kama tarehe ishirini na na nane hivi, mwisho wa mwezi huu. Na ndio mmesikia kuwa kwa kila wilaya mmechagua nyinyi wenyewe watu mnaotaka, wenye watakuja kuwaakilisha kule. Na basi tuna furaha leo kuwa na muwakilishaji wa kwanza nitamwaomba asimame tena iliniwaone. Huyu muwakilisha anakuja, ingawa atakuja kuwaakilisha akina mama, lakini anakuja kuwaakilisha maoni ya watu wa Trans Nzioa. Kwa hivyo, mtu mwenye mtanakiwa kuwasiliana naye kwa njia ya karibu. Wale wawili hata mimi bado sijawaona ingawa nimekuwa sehemu ya hii wilaya nitarudi pila kuwaona, waeleze wananchi juu ya waakilishi wao.

**Emmanuel Satia**: Asante, wale walio chaguliwa hawa watu wa Cherengani ni kama wakuwa na bahati sana, kwa sababu yule mwakilishi mwingine anaitwa Isaack Subei naye ni wakili hapa mjini, nimeambiwa baadaye kwamba yeye ni mtu wa Cherengani sijui kama ni ukweli?

**Audience**: Ni ukweli

**Emmanuel Satia:** Yule mwingine wa pili, anaitwa Bwana Nathaniel Thuo naye ni manager mkuu wa …………..(inaudible) sijui kama mnamfahamu?

**Audience:** Ndiyo

**Emmanuel Satia:** Sawa sawa na ninaambiwa pia yeye ni mtu wa Cherengani, Okay Asante.

**Com. Salome Muigai**: Sasa tunajua wajumbe wetu na tunawajua waakilishaji wetu, na pia pengine jina la wajumbe tumelitumia kwa wanasiasa wetu. Lakini mjumbe ni yule mwenye kuwakilisha ni kam .leo ni siku yenye tutajifunzi kiswahili

sanifu. Kwa hivyo wenye tunajua kama mjumbe huku mbali tunajua kwani tunaendelea kujifunza kiswahili sanifu……………….. (inudible)

Kabla sijazumzia habari ya Katiba ya leo, ningependa tena kuwaeleza kuwa Kati ya reports tumetengeneza, tumetengeneza pia report ya kutoka hapa hapa Cherengani, kwa hivyo tuna Cherengani Constituency Report, na iko kwa office ya coordinator. Kwa hivyo ukitaka kwenda kuingalia wenzangu kutoka Cherengani kwenye kikao Bunge cha Cherengani ya kitamaduni, unaweza kwenda, utasoma hiyo report, kwenye ofisi ya coordinator. Nafikiri kufikia sasa mnajua pahali ofisi ya coordinator wenu ilipo. Mnajua? Mnataka awaeleze tena?

**Audience:** No, atueleze.

**Com. Salome Muigai:** Okay waeleze.

**Emmanuel Satia:** Asante sana. Kwa wale wasiojua, office yetu iko katika nyumba ya. Sacco office numbari thelathini na tano

**Com. Salome Muigai**: Sasa sijui kama umeshawaelezea mahali ofisi iko? Sasa mshapatiwa nakala ya hii Katiba mpya na ningetaka tuendwe kuwafanyia Introduction. I am just going to introduce it. Nitawafanyia tu introduction, introduction inaitwa aje? Utangulizi?

**Audience:** Utangulizi

**Com. Salome Muigai:** Utangulizi, si niwambia hili ni darasa la Kiswahili**.** Nimeanza sasa

**Audience**: Wengine hatuna.

**Com. Salome Muigai:** Ikiwa tafadhali unayo tumia na mwenzako aliye karibu nawe, sifikiri kama tunayo ya kutosha kila mtu. Tafadhali ukiwa unayo angalia na mwenzako aliye karibu nawe. Na ikiwa uko pahali kwenye hakuna hata mmoja tafadhali songa karibu na pahali kunayo. Kuna nakala za huku zenye tunazo na tutaleta. Nitaanza,

**Audience:** Kiswahili.

**Com. Salome Muigai**: Nani mwenye haelewi Kiingereza

**Audience:** Ni wengi sana.

**Com. Salome Muigai:** Hata kidogo, inua mkono kama uwelewi kingereza, okay, basi wale wengine nani anaelewa kiingereza, hawa wenye tunaelewa kingiereza kazi yetu moja ni ya kutafusiri kwa pamoja ili tuweze kuelewana kwani ile document yenye niko nayo na ndiyo yenye kila mtu amepata. Maandishi yenye niko nayo mimi mwenyewe nitazungumza kwa Kiswahili. Mimi mwenyewe nitazungumza Kiswahili lakini vile nitasema nikisema ile nakala yenye tutafuata hata yenye tuko nayo ni ya kingereza. Kwa hivyo hata mimi ninapozungumza Kiswahili, tunaendela kutafusiri. Mngependa kuangalia halafu tutaanza. Neno la kwanza la Katiba ni kuwa, tukupaliane tutakuwa na mikutano mingapi.

**Audience**: Mmoja

**Com. Salome Muigai:** Tunafanya Katiba ya huu mkutano tafadhali kwa hivyo tukija tunawauliza swali la kwanza tunataka mikutano mingapi kwa huu mkutano.

**Audience**: Mmoja.

**Com. Salome Muigai:** Kusema tunataka mkutano mmoja ni kusema aje?

**Audience:** Tuwe na umoja

**Com. Salome Muigai**: Ni kusema mtu anayetuongoza akiwa anazungumza wengine tutafanya nini?

**Audience**: Tutanyamaza.

**Com. Saloem Muigai:** Tutanyamaza na tumsikize. Halafu, kitu ambacho ningependa tufanye ni kuwa mnisikize mimi niendelee kuzungumza, nikiwauliza swali mnijibu mpaka twende moja kwa moja kwenye haya maandishi. Halafu, nita maliza na nitawapa nafasi ya kuuliza maswali ama watu kueleza mambo yale ambayo wanakubaliana nayo. Lakini ni baada ya mimi kumaliza. Najua wengine wanasema kwa nini mwenye kiti anasema hivyo na huu ni jambo wa kawaida. Kuna pahali nitafika kila mtu asikie ni perepetwa lakina perepetwa hakuna, huenda uperepetwa wako njini kidogo mimi nimaliza tuendelee na haya maandishi halafu tukimaliza tuwapatie nafasi ya kuzungumza. Tumekupaliana hayo.

**Audience:** Yes.

**Com. Salome Muigai:** Na tumekubaliana hakuna atakaye zungumza wakati mtu mwingine anapozungumza.?

**Audience**: Ndio.

**Com. Salome Muigai:** Wakati hata tutaanza kuuliza maswali, hata mtu akisema jambo lenye amkubaliani nalo, kutakuwa tu kama vile tulifanya wakati wa kutoa maoni. Wewe utamupa nafasi yake ajieleze yeye alafu akimaliza na wewe ukipata nafasi yako utatueleza maoni yako yatokea kwa sauti kubwa. Lakini ni lazima tupeane heshima ya kunyamaza na kusikiza. Kila mtu ananisikiza kutoka mbale nyuma? Mnanisikia kutoka pale nyuma, mnaelewa Kiswahili changu?

**Audience:** Tunaelewa.

**Com Salome Muigai:** Okay, sasa ningetaka zote tungalie mda wa msuada na tunaanze na ukuraza wa pili pahali penye sisi wenyewe tulikupaliana kuwa, popote tulikoenda mlituambia kuwa Katiba ijayo mngetaka iwe na utangulizi ama iwe na Preamble. Mnakumbuka wengine wakisema hivyo kwenye kikao hivyo? Mnakumbuka watu wakisema tunataka Preamble ama tunataka utangulizi"

**Audience**: Ndiyo

**Com Salome Muigai**: Sasa kwenye Katiba Mpya tumeweka utangulizi na huo utangulizi, unaanza kwa kusema ni nani aliyetengeneza hii Katiba. Na inasema, we the people of Kenya, kwa hivyo nikusema sisi ni akina nani?

**Audience:** Wana Kenya.

**Com. Salome Muigai:** We the people of Kenya ni kusema nini?

**Audience:** Sisi ni watu wa Kenya

**Com. Salome Muigai**: Aware of our Ethic, Cultural, Religious Diversity, kupitia nini? Kupitia makabila yetu, na nini tena?

**Audience:** Mila

**Com. SaLome Muigai:** Utamatuni wetu, na nini tena?

**Audience:** Na dini

**Com. Salome Muigai**: Na dini zetu silizo tofautiana and determined to leave in peace and unity, natukiwa tunafanya nini, tunajitahidi?

**Audience**: Kuishi pamoja.

**Com. Salome Muigai**: Kuishi pamoja kwa amani na pamoja, as one indivisible sovereign Nation.  Kama nini?

**Audience:**  Kama taifa moja

**Com. Salome Muigai:**  Kama taifa moja lisilofanya nini?

**Audience**: Lizilo tawanyika

**Com. Salome Muigai:** Committed to naturing and protecting the well-being, tukiwa tunafanya nini? Ya kwanza mimi niliwaambia, aware of our differences nilitafusiri mimi, sasa hii committed ni kusema nini? Committed nikujitoleatolea kufanya nini?  Kutunza na kulea na kufanya nini pia? Protecting the well being of individuals, kufanya nini?

**Audience**: Kulinda

**Com. Salome Muigai**: Tulinde nini?

**Adience**: Masilahi

**Com. Salome Muigai**: Masilahi ya nani?
**Audience:** Ya kila mmoja

**Com. Salome Muigai**: Ya mtu binafsi, ya family and the community, masilahi ya mtu binafsi  na ya nani mwingine?

**Audience:** Ya jamii.

**Com. Salome Muigai:** Na taifa nzima, kukiwa jamaa,jamii na Taifa kwa jumla, sivyo? Recognizing the aspiration of our women and men.  Ni kufanya nini tena? Ni kutambua nini?

**Audience**: Matakwa

**Com. Salome Muigai:** Matakwa ama nini?

**Audience**: Matarajio

**Com. Salome Muigai:** Matarajio ya akina mama na akina baba, wazee ni wanaume? Wazee ni akina nani, hata akizeeka tuseme tukitambua matakwa na madhilio na maazimio ya wanawake na wanaume. And for a Government based on essential values of freedom, maadhilio ya nini?

**Audience**: Ya serikali.

**Com. Salome Muigai:** Ya Serikali yenye?

**Audience:** Uhuru.

**Com. Salome Muigai**: Uhuru wa nini? Thamana zetu, essential values, thamana zetu, thamana za nini na nini? Freedom, freedom ni nini?

**Audience:** Uhuru

**Com. Salome Muigai:** Democracy ni nini?

**Audience:** Haki

**Com. Salome Muigai:** Social justice

**Audience:** Haki za kijamii and the rule of law, na nini tena, utawala wa kinini?

**Audience**: Utawala wa kisheria

**Com.Salome Muigai**: Utawala wa kisheria. Expressing our Sovereign and Inaliable rights. Haya sasa ndiyo tumefiakia siku ya kiswahili, imeananza. Expressing our sovereign and inaliable Rights, mazoezi ya nini? tukizoea, ikizoea kwa nini, exercising our rights, when I am exercising my rights what do I say in Kiswahili. Tukitekeleza haki zetu za?

**Audience:** Tukitekeleza

**Com. Salome Muigai:** Tukitekeleza haki zetu za nini?

**Audience:** Za kitaifa.

**Com. Salome Muigai:** Taifa huru, to determine na ninaelezwa hapa na kijana kijana msomi, kutongeukisha ama sizizokeukwa, inaliable, yaani ni haki zenye hasiwezi kufanya nini, kukeukwa ama kubadilisha ama kuanjwa. To determine the form of governance, kufanya nini?

**Audience:** Kutambua

**Com. Salome Muigai**: Kutambua ama kufanya nini tena, determine. Kuamua ama kujiamulia aiana ya nini?

**Audience:** Aina ya Government

**Com. Salome Muigai:** Aina ya utawala of our country and having participation of the sovereign. Governance of our Country . Utawala wa nini ?

**Audience**: Wa nchi yetu.

**Com. Salome Muigai:** And having fully participated in the Constitution making process. Na tukiwa tumeshafanya nini?

**Audience:** Na tukiwa tumeshashiriki

**Com. Salome Muigai**: Kwa nini, kwenye nini?

**Audience:** Uhundaji wa Katiba

**Com. Salome Muigai:** Kwenye uhundaji wa Katiba hii, do adopt and enact and give to ourselves. Ati tunafanya nini? Adopt?

**Audience**: Tunakubali

**Com. Salome Muigai:** Ama nini?

**Audience**: Tunaitimiza

**Com. Salome Muigai**: Kubali, kutimiza ama

**Audience:** Anzisha

**Com. Salome Muigai:** Tunaianzisha, tunaikubali and enact and give to ourselves, and enact? Nani amekuwa akifanya nini? Enact, kutengeneza na kuhunda na kupitisha and give to ourselves, halafu tunafanya nini, tukishaiunda na na kuipitisha tunafanaya nini?

**Audience:** Tunajipatia

**Com. Salome Muigai:** Tunajipatia sisi wenyewe and our future generation this Constituion. Tunajipatia sisi wenyewe na akina nani?

**Audience**: Na vizazi vijazo

**Com. Salome Muigai**: Na vizazi vijazo na tunawapatia nini?

**Audience**:Hii Katiba

**Com. Salome Muigai**. Na tunasema Mungu afanye nini

**Adience:** Aibariki Kenya.

**Com. Salome Muigai**:Kwa hivyo hata sasa nani angeta kutueleza hiyo Preamble kwa Kiswahili. Vile tumesema pamoja.

Hii Preamble utangulizi wa Katiba yetu inasema, Sisi watu wa Kenya tukielewa kuwa Kimataifa, utamaduni na dini tofauti na tukiwa tufanya nini, determined, tulisema ni nini?

**Audience:** Tukijitolea

**Com. Salome Muigai:** Tukijitolea kukaa kwa usalama na kwa umoja kama taifa lisilo fanya nini?

**Audience:** Lisilo kawanyika

**Com. Salome Muigai**: Committed, tukijitolea kutunza na kulinda masilahi ya kila moja,ya jamii na jamaa katika taifa letu, tukitambua matarajio ya wanawake na wanaume wetu kuwa na Serikali, yenye msingi wa dhama na uhuru, democracia, haki ya kijamiii na maongozi ya kisheria kwa mazoezi tukitekeleza haki zetu sisizokeuka na uamuzi wa kutekeleza uongozi wa nchi yetu. Na pia tukiwa tumefanywa nini, tumewasilishwa, tumeshiriki kwa uhundaji wa hii Katiba, tuifanya nini, tunaikubali, tunailinda, tunafanya nini tena?, tunaitekeleza na tunajipatia sisi na vizazi vijavyo nini?

**Audience**: Katiba.

**Com. Salome Muigai:** Hii Katiba, na tunasema wote pamoja.

**Audience:** God bless Kenya.

**Com. Salome Muigai:** Mungu aibariki Kenya. Kwa hivyo huo ndio utangulizi wa Katiba yetu na tunatakiwa tufikirie hayo maneno kwa sababu hayo maneno itaendelea kufadishwa kwa hii Katiba kutoka mwazo mpaka mwisho. Kisha tukiangalia sura ya kwanza. Hii Katiba ina sura ishirini.

Tuangalie sura ya kwanza, inasema kuwa Sovereignity of the people and the supremacy of the Constitution. Hiyo maana yake ni nini? Ukuu wa nini? Ukuu ama mamlaka ya nini?

**Audience:** Mamlaka ya watu na ukuu wa nini?

**Com. Salome Muigai:** Mamlaka ya watu na ukuu wa katiba, kuwa watu wa Kenya wenye nini? Mamlaka ni ya nani?

**Audience :** Ni ya watu

**Com. Salome Muigai**: Ni ya watu wa Kenya, inasema pia italinda ukuu, Katiba yetu na inasema vile tutakavyo itengeza Katiba ana vile tutakavyo fanya nini tena? Vile tutakavyo ilinda Katiba. Na inasema pia Sheria za Kenya sitatoka kwa Katiba, zitatoka pia kwa sheria zenye zitaundwa, ukitaka kuangalia hivyo vipengele vyote, viko kwenye ukuraza wenye nitakwambia hivi karibuni kwenye ukuraza wa nine. Vienye inaonekana. Ukiangalia kwenya ukurasa wa nne utapata kuwa kuna mamlaka ya watu katika nambari moja, angalia kwenye nambari mbili utapata ukuu wa nini?

**Audience:** Katiba.

**Com. Salome Muigai:** Ukuu wa Katiba, nambari ya tatu, ni vile tungetekeleza nini?

**Audience:** Katiba

**Com. Salome Muigai**: Nambari ya nne ni vile tutakvyo fanya nini?

**Audience**: Linda

**Com. Salome Muigai**: Vile tutalinda Katiba na nambari ya tano ni kuhuzu sheria za nini?

**Audience:** Za Kenya.

**Com. Salome Muigai:** Na tumesema sheria sitatoka wapi, mwanzo tutatoa sheria za Katiba ama hii itakuwa shera silizoanzishwa ama zilizoundwa kwenya Bunge, zitakuwa sheria za utamaduni wetu, si ndio vile mlindwapia? Mngetaka utamaduni wetu sheria zake pia siwe na sehemu fulani kwenye hii Katiba mpya.

Na pia hii kuna sheria za Kiislam zingine, moja moja siyo zote, nitaeleza zaidi juu ya hiyo na zile zingine zenye sinafahamika kuwa ni sheria zenye sinaweza kukusimamia. Na pia katika (F) kutakuwa na sheria za Africa Mashariki. Unajua siku hizi tumekuwa na hata Bunge la Africa Mashariki, mnaelewa hivyo wakati huu, kwa hivyo hiyo pia sheria ambazo zitatungwa na hilo Bunge pia sitakuwa sheria za Kenya na pia sheria za nchi za international. Hiyo nini? Nchi za kimataifa. Kwani sisi wenyewe Wakenya hatujajipenda kama mataifa yale mengine, sivyo? Tuna uhusiano na mataifa yale mengine kwa hivyo sheria zingine za kimataifa zitatuhusu sisi.

Na tumesema numbari ya pili kuwa tumeipa Bunge miaka miwili ili iweze kutunga sheria zenye sitafuatana na hii Katiba mpya. Hiyo ndiyo sura yetu ya kwanza.

Ukiangalia sura ya pili, inazungumzia juu ya Jamhuri. Inasema kuwa Kenya nini? Ni Jamhuri. Inaeleza pia pahali mipaka yetu itakuwa, inaeleza nini tena? inaeleza mji wetu mkuu utakapokuwa. Tafadhali ingetaka tu pengine kufuata tu ukurasa wa pili pekee yake, wakati tunahitaji kwenda kule ndani tutawaeleza mwende ndani, tuanze na jambo moja lingine lakini, mambo yaliyo hapa ni ya kusomwa jioni, ama siku nzima. Kwa hivyo wakati huu ninawaelekeza tu halafu mtaenda nyumbani, mtu atapata nafasi na kuisoma ile nyingine. Tunaelewa.?

**Audience**: Yes.

**Com. Salome Muigai**: Tukisema tusome kila page ama kila neno tutakuwa hapa kwa wakati mrefu. Tutahitaji siku mbili, tatu au nne hata pengine week tatu. Sisi kutunga hii ilituchukua mwezi mmoja, Mombasa bila kufanya kazi ingine, kuanzia asubuhi, tunaenda wakati mwingene kulala saa nane ya usiku. Tukiandika mambo haya. Kwa hivyo sifikiri kama tunaweza kuangalia kila neno leo lakini huu ni mwanzo tu wa safari ndefu ya Katiba.

Tukirudia kwa ukurasa wa pili, nambari ya tisa, lugha tumesema lugha zetu za kirasmi sitakuwa lugha mbili. Lugha ya Kiswahili na lugha ya Kiingereza. Tumesema pia tutakuwa na lugha ya taifa yenye itakuwa ikipita ndani, Kiswahili. Lakini mbali na hii tumesema kuwa pia hii Katiba inatambua lugha zetu za baba na mjomba. Wakati huu ninaelewa pia lugha ambayo siyo ya baba pekee yake. Kunaweza kuwa lugha ya mama ikiwa tofauti, sivyo? Kwa tumetambua lugha zetu za kiasili na hii Katiba imeomba Serikali kuwekea maanani hizi lugha na kuweza kutusaidia ili tufunzwe na tusisahau.

Tumesema kuwa nchi ya Kenya, taifa la Kenya ndilo taifa la kidini. Yaani hakuna dini moja yenye ni dini ya taifa. Lakini taifa hili linatambua nini? Na linatambua dini zetu tofauti na kila dini, itapazwa kuwa imetoshana na ile nyingine. Tunaelewa hiyo, liwe taifa la dini moja lakini si na dini tofaudi. Kama vile tulivyosema kwa utangulizi. Tunatambua kuwa tuna dini tofaudi. Tunatambua pia kuwa tutakuwa kutakuwa na ishara za taifa letu. Hizi ishara sinapatika kwenye … nitawaele za mahali penye sinapatika lakini sitakuwa ishara zipi, kutakuwa na Bendera ya taifa, kutakuwa na wimbo wa taifa, kutuwa na court of arms, hiyo nini? Ni kirauni, si tumesema kuwa pesa zetu sina kirauni, hiyo tumekubali hiyo kirauni kuwa tutaelewana. Basi tutakuwa na kirauni na tutakuwa pia na muhuri wa Kenya. Kuna muhuri wenye upigwa kwenye karatasi inaonekana kuwa hiyo ni maandishi rasimi ya kitaifa. Tunaambiwa kuwa hiyo iko katika ukuraza wa arubaini na mbili mtaziangalia kwa utaratibu ili mwishowe

Katika sura ya tatu, kuna National Goals Values and Principle. Goals ni nini? Kuna nini ya taifa? Kuna malengo ya taifa, kuna thamana ya taifa na mahadhili ya taifa hicho ni Kiswahili cha Kindani tuko mbali sana na Mombasa. Kitale na Mombasa ni mbali lakini vizuri tuelewe hayo kwa hivyo pengine ya maneno ambayo imeandikwa kwa maandishi lakini sisi wenyewe tukisema tuna goals. Tunaelewa nini. Goals ni nini,

**Audience**: Malengo.

**Com. Salome Muigai**: Na je tukisema tuna goals, tunaelewa nini, goals ni nini? ……..

**Audience:** Dhamana,

**Com. Salome Muigai**: lakini watu wengi wenye hawajui wenye dhamana lakini wanajua values ni kusema nini.

**Audience:** Dhamana ni faida.

**Com. Salome Muigai:** Dhamini, Values, hivyo tukisema mama anaheshima zake, ananafasi yake, baba anaheshima zake ana nafasi yake, hizo ni dhamana, hizotunasita aje kwa jina lingine? Tunatumia dhamana kwa leo, lakini na pia tuelewane. Na pia tuna principles. Priciples ni nini?

**Audience:** Ni msimamo.

**Com. Salome Muigai**: Msimamo, tuna msimamo wetu, tunasema kitu fulani kikifanyika hivi, mambo yetu kwa hii ni kitu fulani. Basi hiyo ndiyo tunaangalia kwenye sura ya tatu. Na pia kwa ajili ya hii Katiba ya leo imetupa uhuru mwingi na imetupa haki nyingi zenye tutangalia mwishowe, tunataka pia kujua tuna uhuru usio na ….. mfano mwingine wa uhuru ni nini? Ama nikiwa

nina haki zangu upande huo mwingine wa haki ni nini.?

**Aundie**: Uhuru na kazi

**Com. Salome Muigai**: Uhuru na kazi, upande mwingine wa kuwa na haki hii ni haki yangu, upande mwingine ni nini? Ikiwa nina haki pia nina nini? Nina jukumu sivyo. Ukiwa ni haki ya kuwa baba, lazima uwe na jukumu ya ulezi si ndio. Ukiwa na haki ya kuwa na shamba, una jukumu ya kulima. Kwa hivyo hakuna kitu chenye lizazi pekee yake. Haki ni upande mmoja wa sarafu, upande mwingine kuna nini? Kuna?

**Audience**: Nguvu.

**Com. Salome Muigai:** Kuna jukumu ama nini ama utekelezaji. Aaa Kiswahili leo. Asiye na Kiswahili sijui atawaelezea nini leo. Sasa hapo tuna jukumu na mwanachi wa Kenya, na jukumu hizi ni nini?

Ya kwanza tunasema inorder to fufill the National Goals and Principles, all the citizens have the principles. Kwanza tungeangalia hayo, hizo National goals sinaseme nini. Ukiangalia ukuruza wa nne, ni vizuri kuangalia haya malengo na haki zetu. Tumesema kuwa kila mtu mwenye anatumia hii Katiba awe ni mtu binafsi, awe ni katika jamii ama ni jamaa lazima angalie haya malengo yenye tumekubaliana. Kuwa jamhuri yetu itatekeleza umoja wetu. Tunakubaliana hiyo ni dhama yetu?

**Audience:** Ndiyo.

**Com. Salome Muigai**: Kuwa Jamhuri yetu itambue kuwa sisi tuna tofauti zetu, siwe za kikabila, za kidini, au ziwe za kuwa tuna wanawake au wanaume, siwe kuna walemavu na watu wengine, kuwa hii Katiba na Jamhuri ita tambua tofauti zetu. Tumeanza na umoja wetu halafu ninakuja kwa nini?

**Audience:** Kwa tofauti zetu.

**Com. Salome Muigai**: Kuwa ingawa sisi ni kitu kimoja, bado katika huo umoja tuna tofauti. Tunaelewa hiyo? Huwa tunaweza kuwa taifa moja na pia tuwe watu tofauti.

Halafu nyingine ni kusema kuwa vile tulivyosema mbeleni kwenye Utangulizi kuwa Jamhuri yetu inatambua haki za kidemocrazia. Hiyo thamana yetu tunakubaliana hiyo ama tunataka Serikali ya mabavu, tunayotaka ni ya nini?

**Audience:** Ya democrazia.

**Com. Salome Muigai:** Ya democrazia. Tumesema pia kuwa hii jamhuri yetu itataka Serikali yenye ni transparent., hiyo ni kusema nini?

**Audience**: iliyo wazi.

**Com. Salome Muigai:** Iliyo wazi, na accountable, hiyo ni kusema nini?

**Audience**: Yenye kuwajibika, kwa hivyo serikali yetu na wana Serikali kila mtu mwenye atafanya kazi kwenye hiyo Serikali, tutamhitaji kuwa transparent, tumesema transparent ni kuwa wazi na tutamhitaji kufanya nini?

**Audience:** Kuahajipika.

**Com. Salome Muigai:** Kwa hivyo hiyo ni matano tu juu ya maelezo yaliyo hapa. Tafadhali ukiwa na nafasi uyasome yote yako mpaka …. Ni mangapi?

**Audience:** Kumi na nane.

**Com. Saome Muigai**: Kwa hivyo tafadhali upate nafasi na tusome hayo mengine. Kuna moja yenye nilikuwa ninataka kusoma. Kumi na mbili, haya huyu baba alijua nitapenda kusoma kumi na mbili. Inasema, the state shall implement the principles that, one third of members of all elective appointment, appointed bodies shall be needed.

Kuwa hili taifa letu, litakubaliana kuwa kwa kila watu waliochaguliwa, kwa watu mia moja, thelathini na watatu watakuwa nini?

**Audience**: Wanawake. Hiyo tunakubaliana.

**Com. Salome Muigai:** Hiyo tunakubaliana?

**Audience:** Hapana

**Com. Slaome Muigai**: Hamjakubaliana,si tulisema tunataka Serikali ya kidemocrasia, Democrasia ina maana gani?

**Audience:** Ni sawa.

**Com. Salome Muigai**: Lakini nauliza Democrasia ina maana gani? Democrasia inasema kila mtu ni lazima awaakilishwe? Sasa mnataka kuwaakilisha waumme pekee yao? Lakini nauliza democrasia ina maana gani, democrasia inasema kila mtu ni

lazima awaakilishwe, sivyo?

**Audience:** Ndiyo

**Com. Salome Muigai:** Sasa mnataka tuwawakilishe wanaumme pekee yao?

**Aaudience:** Hata wamama

**Com. Salome Muigai:** Kwa hivyo tukiwa tunataka dhamana ya democrasia, democrasia inasema kila mtu lasima afanywe nini?

**Audience:** Awakilishwe

**Com. Salome Muigai:** Awakilishwe, naikisema kila mtu, hatusemi mtu mwenye nguvu lazima awakilishwe, au mwenye sauti lasima hafanye nani? Awakilishwe, inasema nani?

**Audience**; Kila mtu.

**Com. Salome Muigai:** Kwa hivyo wengine wanaume waakilishwe, lazima mwanamke afanye nini? awakilishwe, lazima akiwa na ulemavu awakilishwe, lazima mlemavu afanye nini?
**Audience:** Awakilishwe.

**Com. Salome Muigai**: Awakilishwe sivyo? Basi tukikubaliana haya malengo, hatuwezi kusema tunakubaliana saa ile inanifaa mimi lakini ikimfaa mwenzangu……………………

Tulisema tutapanda mahindi, na tutapanda kwa njia hii. Na hatuwesi kubaliana tutapanda kwa njia hii ikiwa inapandwa kwangu, lakini tukiwa tunapanda kwa machine, tupande sehemu nyingine. Ni msimamo. Na hiyo ndiyo mambo yenye tungekuwa tukiiweka dhama, sisemi yale mambo mengine. Kuna mambo mengine yenye hayajatajwa hapo, hasa I think there was something about kutakuwa na mambo mengi baadhi ya masilahi ya walemavu kwenye hizi nakala zetu, kutakuwa masilai ya watoto, kutakuwa na habari ya vikundi vya jamii zilizo ndogo ndogo kwenye hizi dhama zetu. Basi tunatasema, masilahi ya kila mtu kama kwa utangulizi tulisema masilahi ya kila mtu kama nani? Kama mtu binausi, kama jamii, kama jamaa katika taifa. Kwa hivyo ndio tulisema tuelewe huo utangulizi kwani mambo yote yenye yatafanya itafuata huo utangulizi.

Sisemi kuwa lazima tukubaliane, lakini ningetaka tukubaliane kwa principles. Kwa ajili again? Tumesema hivyo, tunaweza kukata kuwa na maoni tofauti kwa utekelezaji, siyo? Lakini ni lazima tu understand tuelewe dhama na zetu pahali tunatoka.

Basi nitakuwa nimeshasoma ya kumi na mbili, tukataja dhamana na tutaendelea sasa kazi za dhama na hizi tutasitekeleza kwa njia gani.

Tunasema kuweza kutekeleza hizi dhama na zetu ni lazima kila mwananchi wa Kenya aweze number (a) kufanya nini? Kujifundisha yeye mwenyewe na wengine hii Katiba inavyosema. Kila mwananchi anawajibu wa kufanya nini? Wa kujifundisha yeye mwenyewe na kufanya bnini zaidi? Kuwajulisha wengine. Are together, duties of the citizen, number kumi na tano. Tuko kwa number kumi na tano (a) uphold themselves to the questions of the Constitution and propagate with ideals and objections. Lazima mimi mwenyewe nijijulishe na nifanye nini? Niwajulishe wengine.

(B) Uphold and defend the Constitution. Lazima nifanye nini? Lazima mimi mwenyewe nifuate hii Katiba na nifanye nini tena? Ni ilinde, unaweza kulinda kitu chenye wewe mwenyewe hufuati. Nakumbuka zamani walimu walikuwa wakitupiga tusivute sigara na yeye anashika kiboko na mkono moja na anavuta sigara na yule mwingine. Unaweza fanya hivyo?

**Audience:** La

**Com. Salome Muigai:** Kifanya hivyo vile unavyoambia watu watasikia?

**Audience:** La**.**

**Com. Salome Muigai:** Hata sisi wazazi wenye tumekuwa tukifuta sigara tunajua vijana wetu lazima pia wafanye nini? Wafuate wakati mwingine, kwani tumewapa maneno lakini vitendo vyetu vina kuwa nini?

**Audience**: Tofauti.

**Com. Salome Muigai:** Tofauti, kwa hivyo tunaambiwa na hii Katiba mpya kuwa ni lazima sisi wenyewe tufuate Katiba na tuifanye nini tuilinde.

(C) Lazima kila mtu mmoja wetu, mwana Kenya afanye nini? Ashughulike kufanya kazi fulani. Kwa hivyo, hii Katiba itatukubalisha kuwa wazembe? Mzembe anaweza kujenga taifa? Mzembe atajenga jamii, atalea mtoto atakayejenga taifa hili? La. Kwa hivyo inatujulisha kufanya nini, tufanye kazi kwa usalishaji wa mali na kwa kufanya nini tena? Na kufanya nini? home making, hiyo ni kazi yenye inatambuliwa kuwa kazi ya nyumbani ya ulezi wa jamii ni kazi yenye inatambulika kwenye hii Katiba. Tunasema we Should work, include home making for the support and welfare of the State and their families for the common good and to contribute to National development. Kwa hivyo tunasema kila mtu atajifundisha kwa kazi hasa ya kufanya nini? Ya kutengeneza jamii nyumbani. Mtu atafanya kazi kwa masilahi ya nani? Yake yeye mwenyewe, jamii yake, jamaa na taifa lote kwa jumla. Huo ni wajibu au mawajibu yenye tunapewa na hii Katiba mpya na hayo ni machache tu yameendelea mpaka (M),

(M) Nambari ngapi? Kumi na nne? Na ningetaka kila mtu apate nafasi ya kuyasoma yote lakini leo ilikuwa mhutasari tu.

Kwa hivyo hii Katiba mpya inampatia mwananchi wa Kenya, Values, Principles ama msimamo, inampatia pia jukumu. Na angalia kuwa tumekuja kwa jukumu kabla hatujakuja kwa haki zetu. That is a deliberate thing. Mpangalio huo umeleta jukumu kabla ujaleta nini? haki zetu. Kwa hivyo tusijukulie haki zetu tuzianze na kuchukua nini? Kabla hatujachukua haki zetu tuchukulie nini? Wajibu wetu ama jukumu zetu.

Page four, ama sura ya nne, inatuletea habari ya uraia. Nani raia wa Kenya , inatueleza mambo matatu, inasema kuwa inatufundisha vile mimi nikiwa raia wa Kenya, ninaweza retention, inatueleza vile tunaweza kuifadhi uraia wetu na vile tunaweza kuupata uraia ikiwa wewe siyo raia, unawezaje kupata uraia. Inatueleza pia kuna watu wenye ni raia kwa ajili wemefanya nini? Wamezaliwa kwenye hii nchi na pia kuna watu wenye ni raia kwa ajili ya nini? Ya kuoa ama kufanya nini? Kuolewa. Ningetaka kuzungumzia kidogo juu ya hiyo. Kwa Katiba iliyoko sasa Mkenya mwanamme akimuoa bibi mgeni, huyu bibi anapata kapatiwa uraia. Lakini bibi wa Kenya akiolewa, ama akioa, bibi anaoa ama anaolewa?

**Audience:** Anaolewa.

**Com. Salome Muigai**: Anafanya nini?

**Audience:** Anaolewa.

**Com. Salome Muigai**: Wanaoana, bibi wa Kenya akiona na mgeni, Katiba ya leo haikubali huyo mgeni kuwa raia. Hata zaidi ya hayo, watoto wenye kutoka kwa hiyo ndoa sio huwa sio wakenya. Lakini tulipokuwa tukizungumza na watu vile tuliambiwa ni kuwa tungetaka usawa wa kihaki. Equal rights, kwa hivyo Mkenya ajieleze akioana na mgeni, tungetaka huyu mgeni apate nafasi ya kuwa raia wa Kenya. Na hasa hasa hata zaidi ya hayo, tungetaka mtoto yeyote aliye zaliwa na Mkenya akuwe na haki ya kuwa Mkenya, awe amezaliwa nas Msichana wa Kenya ama awe amazaliza na mvulana wa Kenya, huyo mtoto apate nafasi ya kuwa ria wa Kenya.. Pia hapa tumeelizwa vile ninaweza kuwa raia kwa kujiandikisha, mtu gani atakaye patiwa uraia wa kujiandikisha. Halafu tulisema pia mtoto yeyote asiye akiokotwa ndani ya Kenya na awe ana miaka nane au kumi, atafanywa kuwa ria wa Kenya. Hakiwa hajulikani alitoka wapi, hajijui yeye mwenyewe, lakini amepatika katika nchi yetu na yuko chini ya miaka nane, tutamfanya kuwa nani? Mkenya watu watuhuliza kwa nini miaka minane, tuna wakati mwingine tutaende tusema watoto wa Kenya lazima wataenda shule na itakuwa ni kwenda shule ni lazima. Kwa hivyo, watoto watakao kuwa chini ya miaka minane si ni mtoto wa kwenda shule, na sasa tutamfanya Mkenya na tutampeka shule.

Tulizungumzia tena na watu wengi tena zaidi sana kwenye mipaka, kwenye majamii zinazo kakaa karibu na mipaka sana sana kati ya Wabukusu, Wateso, watu wengine gani wako kwenye mipaka yetu? Masaai,

**Audience:** Masaai,Waturukana

**Com. Salome Muigai**: Waturuka wako kwenye mipaka yetu, Wasomali,

**Audience:** Wadigo,

**Com. Salome Muigai:** Wadigo, wako wapi na wapi, Tanzania na hapa ama?

**Audience:** ndiyo.

**Com. Salome Muigai**: Okay, walituzungumzia sana hali ya kuwa kuwa, wao wenyewe wana jamii upande ule wa mipaka na upande huu. Kwa hivyo, walizungumzia sana kuwa hii Katiba iwape nafasi ya kuwa mtu anaweza kuwa raia wa nchi mbili. Na wakasema msipo kubali, ni ukweli kuwa sisi ni raia wa nchi mbili. Tulipata watu wenye walifuata wakati wa uchaguzi wa Uganda ni moja wenye walisimamia kiti cha urais alikuwa nani?

**Audience:** Awori

**Com. Salome Muigai**: Na wenye wanataka kuwa ria wa Kenya, mmoja anaitwa nani? Anataka kuwa Rais wa Kenya anaitwa nani?

**Audience:** Awori.

**Com. Salome Muigai**: Awori, awa Awori wawili ni watoto wa baba na mama mmoja, mnajua hivyo. Kwa hivyo ni ukweli kuwa tuko watu wa nchi mbili. Kwa hivyo hii Katiba mpya inapendekeza watu kukubaliwa kuwa raia wa nchi mbili. Na nyinyi wenyewe pia kuna watoto wenu nchi za ngambo, wengine wamepata green card wakawa ni wenyeji wa America. Na siku moja kama wangetaka kurudi, mngetaka wafungiwe?

**Audience:** Hapana.

**Com. Salome Muigai:** Kwa hivyo, hiyo ndio inazungumzia juu ya kuwa dual citizen, yaani citizen wa nchi mbili. Tumezungumzia vile unaweza kupoteza uraia wako, na pia tumezungumzia habari ya pahali penye unaishi, tumeizungumzia jinzi gani tunaifadhi kuusiana na uraia na tumeizungumzia kuwa kuwa tutaanzisha chama kitakacho itwa Citizen Chief Registarion Board. Ili kuangalia shida yingi zilizoko kwa habari ya uraia. Hata kwa kabila hizo zenye kuishi kwenye mipaka.

Sura ya tano twazungumzia the Bill of Rights. Bill of Rights ni nini? Mswada wa haki za binadamu. Hii ukurasa umeeleza mambo

mengi sasa juu ya haki. Sasa tumeshajua juu ya dhamana zetu ni zipi, wajibu wetu ni upi, sasa tunataka kujua haki zetu ni zipi.

Tunazungumzia wajibu sasa wa taifa ama wa serikali kwa mwananchi wa Kenya. Nimesema kuwa kuna haki fulani na tuna uhuru fulani wenye tumepatiwa na Katiba, inaeleza kuwa hizi haki, kuna haki yenye haina kisogo? Tunaweza kupata haki isiyo na kisogo? Kuna haki, hakuna haki isiyo na kisogo. Wakati Pakastan ilipoanza kuwa na Katiba yao, yeye alikuwa ni mwanafunzi wa Sheria Pakastan, na wakati watu wa Pakastan walipo pata Katiba yao walikuzia watu uhuru kabisa. Kwa hivyo, walikuwa wakitembea barabani wakirusha mikono yao. Kanyaga nchi yako kwa nini? Kwa nguvu na nini? Na raha. Kwa hivyo hawa wakikanyaka nchi yao na kuinua mikono yao walikuwa wakienda na kutoka………mapua yale nyingine yenye kuja upande huo. Mpaka walipo enda hakima wakili akasema haki yako ya kuendesha mkono wako vile unavyotaka, inamalisikia pahali bua langu linaanza. Ndio haki yako ya mkono wako usitatize nini, pua langu. Kwa hivyo, hii Katiba ya leo imetuzungumzia pia pahali gani kisogo cha haki hizi ziko. Tafadhali uinganalie.

Imezungumzia pia haki ya kuwa hai. Haki ya kuwa hai, wewe upatiwi haki ya kuwa hai na wanadamu wenzako ama na serikali. Kwa hivyo hakuna mtu mwenye ana haki ya kuitoa. Rights to life ni fundamental right, ni haki ya kuwa wewe ni mwanadamu kwa hivyo hakuna Serikali ama mtu aliye na haki ya kuichugua. Kwa hivyo, tumeondoa adhabu ya kifo. Usiseme tunakubatia haki ya kusema huna haki ya uai alafu wakati mwingine tunasema hiyo haki inaweza kuondolewa. Watu wengi wamekuwa katika kiza ya kuwa tumetoa haki ya kifo, lakini tulipo zungumza sana na jamii mbali mbali, tulishutuka kuelezwa kwamba, makabila mengi ya Kenya haikuwa na adhabu ya kifo. Mtu alipoua mtu wa jamii fulani, hiyo jamii ililipwa ridhaa na ile jamii nyinge, kwa namna moja ama mbili. Mimi jamii yangu ilinikarisha kabisa kwani naambiwa jamii ya Kikuyu, kama ukiua mwanamke, ulikuwa unatoa ridhaa ya kondoo thelathini. Lakini ukimvuja mtoto mvulana mguu, ilifanyika ridhaa ya kondoo ya hamsini. Na hiyo haikunipendeza hata kidogo. Lakini vile tunataka kusema ni kuwa, hii habari ya mauaji ati mtu mmoja ameua kwa hivyo naye auawe, hakuwa kwenye mila zetu. Sijui mila za hapa zilikuwa sikifanya nini? Mtu alipoua, alifanywa nini?

**Audience:** Alilipa fine.

**Com. Salome Muigai:** Alilipa fine au ridhaa.

**Audience:** Alipa ng’ombe

**Com. Salome Muigai:** Hata mwenye alikosa hiyo ridha, kama jamii yako haikuweza pahali pengi huyu mtu akifukuzwa, lakini hakuuawa. Ni Kweli?

**Audience**: Ndiyo, alikuwa anatengwa.

**Com. Salome Muigai**: Alikuwa anatengwa, lakini hauawi. Pengine hapatiwi kitu, pengine akifa anakuwa huo ukoo yakua

imefanya nini imeisha. Lakini hakufanya nini? Hakuuawa, kwa hivyo tunarudia siku za zamana zetu na tumeondoa adhabu ya kifo kwenye Katiba yetu.

Tumezungumzia sanahaki, uhuru wa kukosa kubaguliwa. Tumesema hii Katiba mpya, haikubaliki mtu kubaguliwa na mwingine ama na Serikali ama na jambo lote lingine. Haukubaliki kubakuliwa na kabila lako, kwa jinzia yako, ama kwa jili ya wewe ni mwanamke ama ni mwanaume, au mlemavu ama siyo mlemavu, kwa dini ama kwa lolote lile. Na ukifikiria umepaguliwa unaweza kwenda kortini kusema una hakika kuwa umebaguliwa.…….. hiyo ya haki sina wasiwasi yeyote kuwa kila mtu atasoma. Kuna mtu mwenye hataki kujua haki zake. Inua mkono kama hutaki kijua haki zako? Nani anataka kujua haki zake? Inua mkono tukuone pia. Wengine hawataki. Mimi ni mwalimu nimezoea kuona mikono, tafadhali nifurahisheni kwa kunionyesha. Okay, kwa hivyo hiyo ni sura moja yenye ninajua kila mtu atasoma.

Tumefikira, na tukazungumzia na tukatafakari sana sana hii ya haki za akina mama. Tumefikira haki zao na tukasileta kwenye Katiba. Pia tumefikiria na kutafakari juu ya haki za wazee wetu wakongwe. Tumefikia wakati wenye, kwa ajili ya watu kwenda kuishi mjini na watoto saa ingine kuondoka sasa vijijini, wazee wetu wanahitaji kufikiria umpya ni kweli? Tunasema ni jugumu la kila mtu kufanya kazi, mnakumbuka tulisema kila mtu afanaye kazi, na aweke mpangaliyo wa vile atakavyo jimutu akiwa mzee. Lakini ikiwa hata anataka kufanya hizi kazi zote na kufanya hizo zote hawezi akiwa mzee basi tutaiweka kuwa jukumu ya Serikali ya kuakikisha kuwa huyu mzee mkongwe ana pahali pa kuishi, ana chakula cha kutosha na na ana matibabu ya kumtosha. Nani angetaka tutoe hiyo? nani hatakuwa mzee? Hiyo ni njia moja kila mtu wetu yuko kwenye hiyo barabara.

Tumefikiria pia habari ya haki za watoto. Haki nyingi za watoto kumbe wakati mwingine tunasikiuka, tunafanaya kwa mfano, kutofikira mambo ya watoto ama maslahi yao, tunafikiria sisi wenyewe tunayajua vizuri na hakuna haja ya kuwauliza watoto. Hii Katiba inasema, tukiwa tuna jambo lenye lina huzu mtoto, na huyo mtoto aulizwe, na maoni yake tuwekee maanani. Hatusemi ifuatwe, kwani mtoto naye pia ana mambo mengi yenye haelewi? Si ni kweli? Lakini ahusishwe. Mtoto akisema hataki kwenda shule fulani, unataka mzazi umsikize. Pengine huyu mtoto anatatizo la namna fulani, lenye hajiweza kueleza, lakini akijua kuwa akieleza atasikiwa, na maoni yake itawekwa maanani, atajieleza. Si ni kweli, kuna mtu mwenye hataki kueleza mambo yake akijua atasikizwa, hilo ni jambo moja.

Jambo lingine ni kusema kila mtoto ana haki ya masomo ya lazima na ya bure. Lakini tunasema masomo haata ikiwa ya bure ni lazima ifanywe kwa lazima? Watu wengi wanafikiri masomo ikiwa ya bure kila mtoto ataenda shule. Ni kweli? siyo kweli. Tunaona saa ingine tunapewa mtoto wa miaka kumi na mbili shuleni tunamuoza. Mtoto wa miaka kumi na mbili ni mtoto sivyo. Sasa tena pia tusema mtoto ni kutokea umri gani? Hadi kumi na minane na kanisa la la catholic wenye kusema sijui mtoto ameanza wapi, badla kusema tukitoa hiyo nafasi mpaka miaka kumi na nane. Yeyote asiye wa miaka kumi na nane, ni mtoto. Kwa hivyo ukipewa msichana wa miaka kumi na saba, uende umuoze, hiyo utakuwa unakeuka nini haki za huyo mtoto na unakeuka sheria za Katiba. Na tulisema wajibu wa kwanza ni kuielewa Katiba na kuifuata na kuitekeleza. Kuna haki nyingi za watoto silizo hapo, waalimu wamekuwa na shida na sisi kwa kusema watoto wasijapwe. Lakini kumbe sisi tulienda shule na

tukachapwa na tangu wakati huu ulisikia mtoto amekufa kwa kujapwa?

**Audience:** Hapana

**Com. Salome Muigai**: Siku hizi tunasikia watoto wamekufa?

**Audience**: ndiyo

**Com. Salome Muigai**: Tunasikia watoto wako Hospitali, unasikia watoto wamevunjwa mguu ama mkono. Kwa hivyo huu ni wakati mwingine na Kitabu cha Mungu chenye mimi husoma kwani ni bibilia inasema, ikiwa na mvinyoo mpya, unaweza kuliweka kwa lile chupa lizee?

**Audience**: Hapana

**Com. Salome Muigai**: La kwa hivyo tuko kwanye wakati mpya huu ni mtindo mpya itahitaji lichuba gani?

**Audience**: Litahitaji lichupa mpya.

**Com. Salome Muigai**: Tunaenda pia kwa haki ya jamii. Familia ndio jamaa ama ndio jamii? Jamii ni community, kwa hivyo jamaa ni family………Basi Constituion mpya Katiba mpya inaangalia haki za jamaa. Imeangalia pia haki za wasiojiweza ama watu wenye ulemavu. Ninafurahi kuwa bado manatengeneza hii hall. Tukija wakati mwingine kama mmeweka steps ishirini, tutakuja kuwashtaki. Mmoja ya haki yenye mtu mwenye ulemavu ni kuwa nyumba zote zinazoweza kuingiwa na raia na kila mtu, public offices and buildings, ni lazima limwezeshe kila mtu kuweza kuingia. Kwa hivyo, ninafurahi kuona bado mnaunda hapa. Na wakati mwingine nikija nitakuta kila rangi. Na mtu mwingine akija na gari la wheel chair anaweza kufanya nini kuingia. Na hilo ni moja tu ya hayo mambo. Tumesema watoto wenye ulemavu, ni lazima tujaribu iwezekanavyo waweze kusoma na wengine bila kutengwa. Kwa hivyo mashule yetu tutahitaji kuwaweza hawa watoto kusoma kwenye hii mashule ya kawaida. Kwa sababu gani? sababu ya kwanza ni kuwa hawa watoto ni wa jamaa na jamii si ndio, tukiwaondoa na kuwapeleka Thika wanakaa huko miaka kumi na miwili. Wakirudi kwa hii community ama hii jamaa tunawajua? Na asiye kujua hakufanyi nini?

**Audience:** Hakudhamini.

**Com. Salome Muigai:** Hakudhamini, kwa hivyo kama tunataka kuwadhamini watoto wetu ni lazima wafanye kazi yetu. Kwa hiyo tunapojenga shule lazima tufikirie kuwa hii shule tunaijenga kwa kurahisisha masomo ya watoto wetu, wawe wana ulemavu ama hawana. Hizo ni dalili tu za mambo yaliyo katika hicho kipengele tafadhali angalieni tena muone mambo gani mengine yako huko.

Tunataka watu wakae na heshima zao, human dignity tunalinda heshima za kila mmoja. Tutataka pia uhuru na usalama wa kila mtu ulindwe na Katiba. Tunataka kila mtu asiye mtu mwenye yuko katika hali ya utumwa, katika hali ya kufanya kazi isiyo na mshahara ama kufanya kazi za nguvu. Hakuna mtu mwenye atalazimishwa kufanya kazi kwa nguvu. Tunataka privacy ya kila mtu ilindwe privacy ni nini? Siyo siri?

**Audience:** Ni siri

**Com. Salome Muigai:** Ni uhuru wa kuwa kwa nyumba yako na usikie hiyo shida yako hakuna mtu mwingine mwenye atatoka kule na kuja kuingialia tu ovyo ovyo. Kuwa wewe ukiwa mtu uko kwa nyumba yako, hiyo nyumba imapatiwa mamlaka yako, na imepatiwa heshima zake. Hakuma mtu mwenye atatoka tu huko kwa ajili ya jambo moja ama lingine aweze kuingilia zile jumba kusio na sababu kamilifu.

Tunataka pia kulinda dini zetu, kutakuwa na uhuru wa kuabudu na wakuamini. Tunataka uhuru wa kujieleza. Freedom of expression, na hiyo pia freedom of expression ina kikomo chake. Unaweza kujieleza na uzungumzie watu uwaeleza mambo yote, maradi tu, isieneze chuki, habari zenye sinaweza kufanya watu waanze vita, na izimalize usalama wa watu. Kwa hivyo katika huo uhuru bado tuna jukumu fulani, una uhuru wa kujapisha maoni yako,una uhuru wa kuwasiliana na kila mmoja unayetaka, una uhuru wa kukutana, una uhuru wa kuandamana na una uhuru wa kusimama ueleze watu vile ungetaka wajuwe. Kwa mafano tukiwa tunapita pale, na wewe unafikiria kuna jambo moja lenye unaweza kutueleza, unaweza kutusimamisha utueleze. Fidgeting, ata unaweza kufunga njia kidogo, lakini mtu akitaka kupita ni lazima umkubalishe kufanya nini? Kupita, umsimamishi kwa nguvu. Na una haki ya kufanya petition. Hiyo ni kufanya nini?

**Audience:** Rufani

**Com. Salome Muigai:** Ni rufani lakini siyo ya kortini. Sisi wote tukisema hatutaki wakati mwanatume Salome Muigai alipokuwa kwetu alituoji, na hatumtaki tena, tunaweza kujukua sahihi za watu wa kikao hiki tumpelekee Yashi Pal Ghai. Tumwambie siku nyingine ukitaka kutuma wanatume kwetu, uakikishe utatuma nani? Salome Muigai, na sababu zetu ni moja mbili tatu, na nine na hizi ndizo signatures za watu wenye tumekubaliana. That is a petition ya nitatuma tu petition. Mkitaka kusema msitu wetu wa pahali fulani hatutaki ukatwe, tutatumia hiyo petition. Hiyo ndiyo haki ya kuwapa uhuru wa kufanya petition. Mnaweza kumpelekea Waziri na mkachukua sahihi za watu fulani , mkapeleka mkasema hii baadhi yetu hatutaki mti yetu ikatwe kwa ajili ya sababu hii na hii na sisi wenye tumekubaliana sahihi zetu ndizo hizi. Mnaelewa? Kwa hivyo hiyo haki pia iko kwenye Katiba.

Kuna haki za kisiasa, kila mtu anahaki ya kuusika kwenye siasa. Kuna uhuru wa kutembea popote Kenya na kukaa popote Kenya. Ukisikia masilahi yako hapo haijukuliwi maanani, na ufikirie kama ningeenda Murang'a, ama Mt Kenya iko karibu

Mungu wa Akikiyu ndiye anayeishi, pengine huyo Mungu ananielewa kuliko kuliko Mungu wa Mt. Gani? Mt gani iko karibu na nyinyi?

**Audience**: Elgon.

**Com. Salome Muigai**: Elgon, huyu Mungu wa Elgon, si pia tuna Mungu Mwingine hapo Elgon? Wa jamii fulani?

**Audince:** Ndiyo.

**Com. Salome Muigai**: Ukisikia huyu Mungu hakuelewi na kutoka leo ningetaka kujaribu Mungu wa Wakikuyu, kwa hivyo nitachukua virago vyangu niende wapi ?

**Audience:** Ukikuyuni.

**Com. Salome Muigai:** Kikuyuni Nyeri karibu na Mt. Kenya ndivyo anielewe vilivyo. Una uhuru wa kufanya hivyo, una uhuru wa kutembea huko na una uhuru wa kuishi kule, mradi tu uishi kwa usalama na wenye utafanya nini? Wenye utakuta kule. Wakimbizi wenye watakuja hapa kwetu kuomba bahali pa usalama, pia wamelindwa na hii Katiba. Kukiwa kama sasa tuna shida sisi wanakenya tumebarikiwa kabisa hatujaweza kukimbia twende tukatafute usalama pahali pengine. Lakini watu wengi wamekimbilia hapa kwetu kuomba nafasi ya usalama. Basi hao wakimbizi pia wamelindwa na hii Katiba.

Uhuru mwingine wenye tunao ni wakufanya biashara na kutafuta kazi, uhuru wa kuwa na mali, kazi, kuwasiliana na waajiri wetu ili tufanye kazi pamoja kwa njia nzuri. Tuna haki ya kuwa na social Security, health fund. Social security nini? Tunalipa Social Security Fund, tunaitaje kwa Kiswahili, wale wenye mnaofanya kazi? Malipo ya uzeeni. Hii ni kusema kuwa kuna haki ya kusaidiwa na Serikali kama hatujiwezi kabisa. Vile tulikuwa tumesema habari ya wazee, ya kuwa mzee mgongwe kabisa amekosa ya kwenda………yeye anahaki ya kuomba usaidizi kwa Serikali. Lakini siye yule mzee pekee yake, wengine wa jamii moja ama mpili, akiwa amejaribua kazi ameshindwa kabisa pengine ni mgonjwa hawezi fanya kazi, tunasema taifa hili lina wajibu kwa watu wake. Ni vizuri muweze kuwa na haki ya kuangaliwa na serikali. Kuna uelewano hapo, lakini siyo tukatae kazi, tunaelewa pia, ndio tulianza na jukumu na jukumu moja ni la kufanya nini?

**Audience**: Ya kufanya kazi.

**Com. Salome Muigai**: Ya kufanya nini.

**Audience**: Ya kufanya nini Kazi.

**Com. Salome Muigai:** Kwa hivyo yule mwenye anashindwa kabisa ndiye tunasema anahaki ya kusaidiwa. Tuna haki ya

matibabu ya afya, kuna haki ya elimu, tuna haki ya nyumba na pahali pa kuishi, tuna haki ya chakula cha kutosha, haki ya maji na usafi. Tuna haki ya mazingira yaliyo salama kwetu na kwa nani mwingine? kwa vizazi vijavyo. Mazingara yetu siyo yetu sisi pekee yetu, ni yetu sisi lakini sisi tunawawekea nani watoto wetu na vizazi vipi?

**Audience**: Vijavyo.

**Com. Salome Muigai:** Vijavyo. Tuna haki ya kutumia lugha yetu na utamaduni wetu. Tuna haki ya consumers rights, hiyo ni ya nani? Ya mnunuzi, haki ya ununuzi. Mtu akiniuzia sugari, ni lazima aniuzie sugari itakayofa kwa matumizi ya mwanadamu. Akiniambia hii sukari ni kilo moja, ni lazima iwe kilo moja, ni lazi iwe kilo ngapi?

**Audience**: Moja

**Com. Salome Muigai:** Hiyo moja aliyo niuzia. Kwa hivyo this are consumer rights. Tuna haki ya kuudumiwa vyema na watumishi wa serikali, hiyo ni haki, fair administration. Tuna haki ya kukosa kutii amri sizizo za sheria. Hii imekuja kwa ajili ya ile janga lenye lilikumba Rwanda. Watu waliuawa sasa mtu akilitwa kortini mwenye aliua atasema mimi nilikuwa nikifuata au kutii nini? Amri. Kwa hivyo wewe kama mwanadamu una haki ya kuangalia kama ile amri yenye unapatiwa ni ya kisheria. Tuanaelewa hiyo, mimi nikiwa sipendi shati la blue, nimeabiwa nimwambie sipendi unajua mimi ni Commissioner nakuambia uende ununue hiyo shati kwani mimi sipendi kuona blue kabisa kabisa, ana haki ya kukataa.

**Audience**: La.

**Com. Salome Muigai**: Kwa Katiba ya leo hana sivyo. Nadhani kwa Katiba hii mpya ana haki ya kusema Madam Commissioner, mimi ninakueshimu, na ninaeshimu vile vyenye unaniambia mara nyingi nyingi, lakini leo, imezidi, hiyo sifuati.

Uuna haki ya kuweza kufikia korti, mahakama, kila mtu ana haki ya kufikia mahakama, leo tumpa mtoto haki ya kufikia mahakama. Mtoto wako akitaka kwenda kukushitaki leo, hataitaji mtu mkubwa ama mtu mzima ndio aende kwa korti. Yeye mwenyewe ana haki ya kwenda kortini aseme, mimi nitaka kumshitaki nani baba ama mama.

**Audience**: Baba ama mama.

**Com. Salome Muigai:** Ama ndugu. Kwa hivyo kila mtu, ana haki ya kufikia kwenye mahakama. Kila mtu aliyeshikwa ana haki zake. Ukishikwa na police unahaki fulani. Ukisoma pale utaona tumesema, tukukalishwa kwenye kituo cha police mda bila kukufikishwa nini? mahakamani. Niko kwenye numbari kumi na nane, hiyo mtaisomea nyumbani. Kila mtu ana haki fulani zenye wakati wa emergency pahali pa kazi, haki zetu sinasimamishwa zingine zivyo. Tafadhali tusiende kwa vipengele vya fifty eight mtavisomea nyumbani ukienda hapo nitakuwaja kwa vipengele vingine.

Tunazungumzia habari ya wakati wa Hatari. Wakati kuna hatari tunaambiwa kuna kazi ya kutoka saa kumi na mbili mpaka saa kumi na mbili asubuhi si ndio? Kwa hivyo sasa tumesema kuwa wakati huu wa hatari, inahaki zake, ina utaratibu wake. Nitaingalia ndio tuone kuwa haki sinasimamishwa kwa mda mfupi iwezekanavyo, siyo kwa mda fulani, ni kwa mda mrefu saidi.

Una haki ya kusema haki zako za binadamu hasijafuatwa, na tumeweka Tume yenye itaangalia hizi haki. Yaani ukukisikia haki zako hujapatiwa, kutakuwa na Tume yenye unaweza kwenda kulalamiakia. Hiyo ndio Tume number seventy three, Tume ya haki za binadamu na to deal with Administrative justice. Administative Justice ni nini? Wenye tulikuwa na Kiswahili kimeisha, na tuko kwa sura ya tano pekee yake na nina ishiri, kwa hivyo tusiishe safari ni ndefu. Itakuwa Tume ya haki za binadamu na kiutawala. Hapo ndipo mahali utaenda kupeleka malalamiko yako. Pia kuna hii tunahaki, ama nguvu za kutekeleza haki zako, yaan mahakama inaweza kukutetea kukiwa haki zako hasijafuatwa na tunaeleza hapo mwisho number 75 vile tutatafusiri hiyo mambo yote. Hiyo nimende kibengele kwa kipengele kwani hapo ndio mto wa mambo ulipo, sivyo, kwenye haki zetu. Sasa twende kwenye sura ya sita. Sura ya sita ni representation of the people ama nini?

**Audience**: Uwakilishaji wa watu.

**Com. Salome Muigai:** Kwanza, hapa tunazungumzia habari ya election, habari ya uchakuzi ningetaka kueleza jambo moja. Tumebadilisha uchaguzi ukabadilika kidogo. Kwa sababu gani? Tulipokuwa tukienda kukuza kusikiliza maoni yenu, watu wenye kuishi zehemu zenye watu wengi kama Cherengani, walituambia hivi:- kikao cha bunge, Constituency siangaliwe tena. Na zipangwe kwa mpangilio wa kuangalia wingi wa watu pekee yake. Hata watu wengine walituabia mnajua wana Tume mjue kuwa waakilishaji wa ubunge sio wa kuwakilisha wanayama, wawe wakiwakilisha nini? Watu, kwa hivyo mtasem watu pekee yao. Tulipoenda bahali kama North Eastern, Mandera, Wajir, Garrisa ama Kajiado na Transmara. Pahali watu ni wachache kwa ajili nayo nchi yao haina mvua kama yenu, watu hawawesi kukaa pamoja na wakapata vyakula, wakatuambia sikizeni wanatume, tukienda kufikiria habari ya Constituencies, mfikirie habari ya urefu na umbali pekee yake, msifikirie wingi wa watu. Sasa hawa watu wenye walitueleza hiyo walikuwa wakenya na watu wenyewe walituambia tufikirie watu waliyoko walikuwa wa kutoka wapi, wa kutoka Kenya.

Sasa vile sisi tupoketi chini tukafikiria, kitu chenye kitaweza kuwasaidia hawa watu wote wawili? Ndio tukasema, mpango wenye tuko nao sasa wa uchaguzi, tumetaka kuibadilisha kidogo, tuseme watu wamachague mbunge wao kwa kupiga kura, lakini pia wapike chama. Kwa hivyo, kura itapikwa mara mbili, unampigia mbunge ana unampigia nini? Chama. Kwa hivyo unaweza kupigia mjumbe na ukapigia chama nyenye siyo chako, hii itasaidia vipi? Hiyo kura yako ya kwanza itampeleka mjumbe mwenye atakuwa number one kwa Bunge. Kura ya pili itakuletea chama. Kwa hivyo chama kitawachagua watu wengine wenye hawakuakilishwa kwenye hiyo kikao. Kwa mfano, hapa Cherengani, kuna makabila tofauti……………………

Mnasema I am a lady, tuelewe kuwa hiyo ni tofauti yetu,………… basi watu wa Cherengani kwa huu utaratibu tulio nao hapa, hata wakijumhika hao wenyewe wote watoke wapige vote wanaweza kumpeleka mjumbe?

**Audience**: Hawawezi.

**Com. SaLome Muigai**: Hawezi, lakini kwa huu utaratibu wenye tumeleta sasa unaitwa mixed member propotion, inasema hivyo. Na kama sasa hata ni kiti kilichi kikibwa ni vyama gani vilivyo vikubwa hapa?

**Audience**: KANU,

**Com. Salome Muigai**: KANU na gani kingine,

**Audience:** Ford Kenya.

**Com. Salome Muigai:** Ni KANU pekee yake, haya, hapa ni KANU pekee yake. Hata tutumie KANU basi. Mkipika kura hapa jamii walio wengi, watampeleka mjumbe kwa jamii yao, si ni ukweli, sasa hiyo intakuwa ni kura moja. Halafu, hiyo yenye tutapikia chama sasa watu wa Cherengani wanaweza kuja kuwaambia KANU, tuliwapatia kura elfu mbili, na hizo kura elefu mbili ndizo zenye zimewapatia nafasi hii ya kuwa chama chenye uhuru, chenye watu wengi zaidi. Sasa hizi kura za ziada, zitaangaliwa, zitakuzwa halafu sitawapa KANU viti vingine vya ziada. Kwa ajili ya ya nini? Ya wingi wa watu wenye waliwapigia kura. Sasa hizi kura za ziada ndizo hii Katiba inasema, hatutaenda kuleta wale wato wenye walikuja kwa kura za Kawaida. Tutatazamia kura za kawaida zimeleta nani. Ikiwa hata simeleta yaani nani mjumbe wa leo, Kirwa, Kirwa anatoka kwa jamii gani?

**Audience:** Nandi.

**Com. Salome Muigai:** Ikiwa mheshimwa Kirwa amekuja kwa kutoka kwa jamii ya Kinandi, na KANU kwa ajili ya watu wa Cherengani kuwapigia kura nyingi, wamepata viti vingine viwili vya siada, basi hivi viti viwili lazima vilete jamii zele zingine.. tunaelewa? Sasa hii itazipatia jamii zote nafasi ya kushiriki kwenye utawala. Ninaona mpaka hapa tukubaliane. Kuna jambo lenye pengine hutakubaliana. Tunasema nusu ya hizi viti, lazima pia ataleta wanawake. Walisema msimamo ni msimamo, wakati mwingine utanifaidi, wakati mwingine utamfaidi mwenzako sivyo. Na kama ni msimamo wetu lazima tuukubali, ukinifaidi ama usipokufaidi. Tumesema hizo viti vya ziada zilete akina mama, zilete jamii zile ndogo ndogo zenye hasitapata nafasi ya kujileta wenyewe kwa wingi wao. Zilete watu wengine kama walemavu, zilete watalaamu pia, kwani wakati mwingi watalamu wetu kama ni wana sheria ama ni madaktari ama ni wana bisharia wenye wangeweza kukusaidia tuwaingize kwenye bunge. Kwa hivyo, saa zingine wakifanya mijadala hata kama ni ya ukulima, tunakuwa hatuna watalamu wa kufanya nini? Wa kuchangia hii habari ya ukulima. Tunakuwa tukifiria habari ya mjadala wa elimu hatuna waalimu. Kwa hivyo hizi kura za ziada pia zilete watalamu wenye uongozi, sasa hiyo ndio watu wengi wanasema tumema the Numbians, watu ninety wasichakuliwe,

watachaguliwa, lakini hawatachaguliwa kwa ajili ya kura zao, watachakuliwa kwa ajili ya kile kitu chenye wanakuja kuchangia jamii.

Pia, kunaweza kuwa na mzee mmoja mwenye heshima sana, anamawaidha mazuri sana, lakini akiambiwa asimame aende campaign kutoka hapa ajue hii constituency imefika wapi, hataweza. Sasa wakati huu wa hizi viti vya ziada ndio tutasema mzee fulani anaweza kuleta kitu mhimu kwenye hii jamii ama kwenye taifa kwa jumla., aletewe hicho kiti na aingie ndani. Tunajaribu kuwafanya watu wengi wausike kwenye utawala. Kwani waswahili husema asiye kuweko lake halipo.

**Aundience**: Halipo.

**Com. Salome Muigai**: Kwa hivyo tunajaribu kupata kila mtu akuwepo. Hiyo tu ndiyo ninataka kuzungumzia. Hiyo ingine ni haki ya kupiga kura, mtu gani atazajiliwa. Tunasema pia mtu gani hatazajiliwa kupiga kura, kura itapigwa kwa namna gani na pia sasa wakati huu mngetaka pia kueleza kuwa, kwa wakati huu kwa Katiba iliyoko ukiwa ujapingwa, ama mtu akiwa hajapingwa wakati mwingi hatupigii kura sivyo? Kwa Katiba hii ijayo sasa tutampikia kura. Kwa sababu gani? Kwa sababu wakati huu wa kumpigia kura ndio pia tutapigia chama. Kwa hivyo tukisema hatupiki kura, kutakuwa hakuna kura Cherengani. Tumepoteza na kazi yetu ya kupikia chama chenye tungetaka. Na sasa nafasi yetu ya kupata hizo viti vya siada ndio mweze kuwaingisha wale wengine kwa hivyo sasa wakati huu kila mtu atapigiwa kura, hata akiwa hana mtu mwenye anampenda

Tumezungumzia habari ya Electral Commission mpya. Tumesema Tume ya uchaguzi itakuwa na wana chama sio zaidi ya Kumi na wasio pungua nane. Tumesema Tume kubwa pengine hatuhitaji., hiyo Tume ndogo lakini iwe na wafanyikazi katika kila wilaya.

Pande nyingine ya hiyo, part two inazungumzia habari ya Electro Commission, hiyo Tume yenye tumezungumzia, inaelezea kazi yake, hii Tume tumeiongeza kazi nyingine moja. Na kazi hiyo ni ya kusajilisha vyama vya kisiasa. Kwa sababu gani, kwa sababu wakati mwingine hii Tume ya ucahaguzi inatoa maswala fulani, kila mara wakija kufanya campaign wanaleta fujo, wakileta fujo mwaka huu na ule, lakini kwa ajili ya hakuwa wasajilishaji, hawana lolote wanaweza kufanyia hicho chama. Kwa hivyo tunasema kwani hao ndio watekelezaji wa uchaguzi, wawe ndio wenye kuwasajilisha vyama. Vyama vyenye havifanyi mipango mizuri, wakati wa uchaguzi, wajue wataenda kuwasiliana na nani, na hao wanatume tena. Hiyo tunajaribu kuleta nidhamu kwenye uchaguzi. Tunasema pia kuwa tumepeana pia hiyo Tume itakaa kwa mda gani, na watu watachaguliwa aje kwenye hiyo Tume.

Kazi ya tatu ni juu ya vyama vyetu vya kisiasa. Tumesema kila mtu anahaki ya kuunda chama cha siasa, tumesema kazi za hizi vyama, tumesema vile vitasajiliwa, na vile vitahitimu kusajiliwa, tusema zile zinaweza kuondolewa, lakini kuna jambo moja tumependekeza. Kuwa vyama vya siasa vipatiwe pesa na Serikali. Kwa sababu gani? Sababu vyama vingine vimekuwa na shida sana kuweza kueleza matakwa yake ama kueleza vile wanataka kwa ajili ya kukosa pesa. Sasa tunasema hivi vyama

vipatiwe pesa. Na tukiwapa pesa, na sisi pia tutawaeleza vile tunavyotaka na hizo vyama sivyo? Ikiwa ni mwananchi ndio mwenye anakuajiri, si lazima naye akueleze vile anataka? Kwa hivyo tunasema hatuwezi kuipatia vyama mitambo ikiwa hatuvipatii pesa. Lakini kitu kingine cha maana chenye watu walitueleza zaidi ni kuwa, hiki kiwaja chenye hivyo vyama vinapigia youth, kandanda, siyo sawa, inaonekana kama wakati mwingine, hiki kiwaja kimeunuka sana upande mmoja. Kwa hivyo chama kingine kikipika mpira kutoka pahali penye kimeinuka, inaenda speed sana kuigia kwa goal ile nyingine. Kwa hivyo tungeta vyama viapatiwe pesa ndivyo viweze kusawasisha nini?

**Audience:** Kiwanja

**Com. Salome Muigai:** Hiki kiwanja cha kuchezea. Haya lakini kuna mambo fulani yenye lazima chama kifuate ndio kiweze kupatiwa pesa. Ya kwanza ni kuwa chama kitapatiwa pesa, kikionekana kuwa ni chama cha kitaifa, siyo chama cha kikabila. Ni lazima hiki chama pia kionekane kwa kura kuwa watu wanakipenda. Kwa hivyo chama chenye hapati 3% ya kura hakitapatiwa pesa zozote. Kwa vile sasa wananchi walikuwa wakiuliza kama kulikuwa na vyama hamsini, vyote vitapatiwa pesa? Hivi vyama hamsini kila moja itapata kura ya 3% la? Kwa hivyo vyama vingine vitaangukia tu kule njiani kwani havitaweza kupita pale. Jambo lingine pengine kwa vyama ni kusema kuwa vyama pia vitapatiwa pesa kulingana na kura zenye zimepata. Ndio pia tunasema ni vizuri upikie chama chako hata kama vikiwa vingi, ni vizuri chama kupikiwa kura ndio kiweze kupata hizo pesa.

Na jambo lingine la muhimu sana kwangu ni akina mama, kama tumepeleka MP wetu wa akina mama, tunapatiwa point moja zaidi. Tumesema ni wakati wa usawa wa haki sivyo?

**Audience:** Wote wapate.

**Com. Salome Muigai**: Mwenye kupata apate itakuwa nini?

**Audience:** Sadaka..

**Com. Salome Muigai:** Sadaka, sasa ninajua watu gani wa rika yangu wenye wanajua wimbo wenye ninajua. Hayo ndio mambo yaliyo katika mswada. Na kuna saidi ya hayo lakini sitaki kwenda kwajili tuko kwa sura ya saba na tutaka sasa kwenda haraka kidogo.

Basi lingine ni Parliament ama Bunge. Mambo mawili nitakayo weza kuizungumzia kwenye Bunge ni kuwa Bunge, tuliambiwa na watu kila pahali tungetaka Bunge lenye vikaoo viwili, kwa hivyo sasa tuna Bunge yenye vikao viwili. Kuna Bunge lenye hawa Wabunge wenye tunachagua wanaenda kukaa, na tuna Bunge lingine lenye litakuwa na waakilishi kutoka kwa kila wilaya, litaitwa Baraza la Taifa ama National Council. Na pia kwenye hili Baraza la taifa kutakuwa na …..kuna wilaya ngapi?

**Aundience:** Kumi na nane.

**Com. Salome Muigai:** Basi itakuwa karibu na watu sabini hivi lakini zaidi, msipotupa wakina mama tutawapa akina mama viti vingine thelathini. Ili ile theluthi, unakumbuka kwa dhamana zetu tulisema kwa kila nafasi lazima akina mama wawe nini?

**Audience:** One third.

**Com. Salome Muigai:** One third, theluthi, kwa hivyo pia, kwenye hizo viti watakuwa hapo. Kitu kingine chenye ningetaka kuzungumzia kuhusu habari ya Bunge ni kuwa Bunge itaanzia kwenye wilaya. Kutakuwa na Bunge ya wilaya. Na hiyo Bunge itachakuliwa na watu na itapata pesa kwa kuitisha koti na pia itapata pesa za taifa. Kwa hivyo badala ya pesa zenye kukuja kwenda kwa kodi, sitakuja moja kwa moja kwenye wilaya. Na hapa pia ndio pahali wilaya itafikiria matakwa yake ni gani ni…..gani muhimu. Kwa mfano, wakati mwingi tukizungumzia habari ya mazao, tunaona tunazungumzia habari ya mazao kama kahawa, majani na parato, watu wa wilaya hii wanakuza nini?

**Audience**: Mahindi.

**Com. Slaome Muigai:** Mahindi. Kwa hivyo ukianza sasa kuawambia habari ya majani, pareto na kadhalika, hiyo siyo ya muhimu kwao. Kwa hivyo pengine Bunge la hapa likiketi, mjadala wa mbele wa habari ya kilimo itakuwa nini?

**Audience:** Mahindi.

**Com. Salome Muigai**: Kwa hivyo hiyo priority, itakuwa tofauti kwa kila wilay akulingana na matakwa yao. Na hiyo ndiyo mambo mawili nitakayosema ya Bunge lakini mambo ya Bunge ni mengi zaidi , tafadhali soma.

Tumesema wabunge watakuwa wakiitimu,kila pahali penye tulienda tuambiwa tungetaka wabunge wenye wamesoma, kwa hivyo tumewakea kuwa lazima akuwe ameitimu daraza ama kidato cha nne. Lakini pia tumesema hiyo haitoshi. Pia ataanagaliwa kwa ajili ya tabia yake, Kwa hivyo mtu akiwa ni mwizi, hata kuwe alipata division ya kwanza, ama (A) kwa kidato cha la form four, hatutamkubalisha kufanya nini? Kutuongoza, akiwa pengine ni mchawi si……..kitu kingine gani, chenye umuhimu jamii yenye inaishi hapa, nani mwingine mwenye hamngetaka awaongoze?

**Audience:** Mwizi, mlevi.

**Com. Salome Muigai:** Mwizi, mmlevi, nani mwingine? mfitini, mfisadi, manasikia, nyinyi tayari mnajua watu gani hamtaki. Jambo lingine ni kuwa, hiyo kutoka mapaka mwisho imezungumzai habari ya Parliament, Parliament hizi zitakuwa namna gani,

itafanya nini calendar yake, hiyo sura ya saba inazungumzia habari ya Parliament…

Jambo moja lenye ningetaka kueleza kwenye page thirty, ni kuwa Parliament tumeizungumzia vile itakavyo undwa na vile itakavyo vunjwa, na nani mwenye atauzishwe kuivunja. Pia ile Parliament italeta mswada wa kutokuwa na imani kwa mtu yeyote au kiongozi yeyote. Mkisoma mtaona vile tumependekeza kukiwa na la ziada tulisome.

Tuangalie chapter eight, yaani habari ya Executive. Ninambiwa iko katika page 19 lakini tusiangalie page 19. Mnisikilize vile tunavyosema, hii chapter yote inaangalia habari ya Rais, Waziri Mkuu, Makamu wa Rais, Baraza la Mawaziri, na mambo kama hayo yaani the Executive. Mambo mawili ama matatu ningetaka kueleza kwani ni tofauti, la kwanza ningetaka kueleza kuwa, Rais bado amebaki na mamlaka mengi, Rais wetu ndiye atakayekuwa amri jeshi mkuu kama vile alivyo sasa. Ndiye mwenye atachagua watu wote wenye alikuwa akichagua kama ni mahakimu, wanatume na mambo kama hayo, ambassadors. Jambo moja tu tuliloweka ni kuwa atawasiliana na Bunge, na watu tofauti. Kama ni wamawakili lazima aulize na wakubaliane na Tume ya kuwaajiri ma-judge ama mahakimu. Kwa hivyo kuna nafasi ya kuwasiliana na watu wengine. Lakini bado mamlaka na ni yake.

Yeye pia ndiye mwenye atatwambia kama tunaweza kupigana na nchi fulani, yaan akuna mtu mwingine aliye na mamlaka ya kuanzisha vita isipokuwa Rais. Na Rais wa huku juu ameanzisha mvua kwa hivyo nitaomba meza yangu kuletwa karibu nanyi. Na nita chukua hiyo nafasi kunywa soda.……ile yenye tumeweka tu la kupendekeza ni kuwa awasiliane na watu wale wengine wake. Si Rais ni baba wa Taifa, sasa akiambiwa awasiliane na watu wake anaambiwa vibaya, hata wazee tutawambia wawasiliane na jamii katika kuanza…mmeanza? Okay sasa hakuna shida hapo.

Mtu mwenye atataka kuwa Rais, atakuja kuomba kura akiwa na mwenzake, running mate, mwenye wataomba pamoja. Na huyo mwenzake ndiye atakuwa makamu wake, kwa hivyo huyo mwenzake atachaguliwa moja kwa moja na wananchi, hiyo ndio tofauti tu kidogo iliyo kwenye hii Katiba. Halafu, chama chenye kitaPata kura nyingi zaidi, kutoka kwa hicho chama Rais atamchagua Prime Minister yaani waziri mkuu. Naye waziri mkuu atawachagua mawaziri wake vile wakenya wengi walituambia ni kuwa, tafadhali mkae chini.

Pahali pengi tulienda tuliambiwa mambo mawili, kuwa wakati mjumbe wetu anapokuwa akiwa Rais ama akiwa waziri, hatutaki mjumbe. Anakaa huko anakuwa waziri huko na anafuatana na Rais na sisi hatupati kumwona mpaka siku ile Rais atakuja kututembelea. Hilo ni jambo moja tuliambiwa na wananchi. La pili ni kuwa, wanataka waziri akuwe mtaalamu wa wizara yake, Hawataki kuwa waziri wa elimu ni daktari na waziri wa afya ni mwalimu. Ama hawataki kusikia kuwa waziri wa kilimo ni daktari ama ni mwana jeshi, ama ni wakili, kuwa wakili na kuwa hiyo mambo yote ni kitu kizuri, lakini mtu aweke utalaalamu wake pahali pake. Kwa hivyo ndio kwa ajili tumesema kuwa waziri asitolewe kwenye Bunge, ndio wakiwa watu wenye kazi yao ni kuendesha nini? Wizara zao, na waziri asiwe akifikiria mambo yake yote atapeleka kwenye kikao chake cha Bunge. Ukiwa waziri kikao chake cha Bunge nini ? Ni wiki nzima, kwani wewe ukiwa ni waziri wa kilimo, unataka kupeleka kila kitu

Kagema kwani ni mbunge wa Kangema. Watu wakikutembelea hata kama ………………(inaudible) ndio kwa ajili tunasema waziri asitolewe Bunge, waziri atolewe nje ya Mbunge, kazi yake iwe ni kuwa waziri wa nchi nzima.

Ya pili, tumesema mbunge naye ajue kazi ya ubunge ni kazi ya kila siku, is a full time job, kuwakilisha watu wako. Usikuwe siku moja wewe ni waziri, siku nyingine wewe ni Mbunge, siku moja hata hujui wewe ni nani, uko hapo kati kati. Shida nyingine yenye wananchi walikuwa nayo kwa kuwa na waziri kutoka bunge walisema kwani kila mtu anaongozwa akichaguliwa waziri, akiwa kuna jambo lenye anahitaji kuwakilisha watu wake, na ni jambo lenye halikubaliki na Serikali, anayetaka kusema ilisikose kuchaguliwa waziri. Kwa hivyo, anaogopa kuwaakilisha watu wake,yeye mwenyewe akingoja kuwa waziri. Kwa hivyo tumesema kuwa mbuge akichakuliwa waziri ni lazima ajiuzulu. Na pia jambo la mwisho, wananchi walitwambia kila mtu afanye kazi ngapi?

**Audience:** Kazi moja.

**Com. Salome Muigai:** Kazi moja, ukifuatwa na hili, moja hufanya nini?

**Audience**: Uponyoka.

**Com. Salome Muigai**: Kwa hivyo ukiwa mbunge kaa na umbunge, ukiwa waziri nawe uwe waziri. Hiyo siju kama inaeleweka.

**Audience:** Inaeleweka.

**Com. Salome Muigai:** Sasa nimezumguzia Cabinet na President na pia wajumbe watatu tu ndio watakuwa wakikaa kwenye baraza la mawaziri**.** Na ni waziri mkuu, na wadogo wake wawili, hawa watakuwa watu wa kukaa kwenye Bunge, watakuwa wabunge. Watu wengi wanasema waziri anawezaje kuwa mtu mwenye tumechagua, waziri mwenye hatuchagua ni rahisi kufukuza kuliko waziri mwenye amechakuliwa, lakini hayo ni mawazo yangu na mnaweza kutupa yenu….

Sasa, niko kwa chapter ya sura ya tisa tuangalie nafusi zetu walio elimika, that explains from Judicial and Legal systems. Hii ni habari ya mahakama, tumesema kuwa mahakama ndio wenye kulinda Katiba ama kulinda sheria, kwani mtu anasikia sheria haijafuatwa lazima aende wapi kwa mahakama. Kwa hivyo mahakama ni lazima wawe thrity na ni wawe na uaminifu. Hauwezi kutulindia sheria wakiwa hawana nini uaminifu. Kwa hivyo tumepatiana mambo mengi juu ya mahakama. Tumepeana pia kuwa na mahakama kuu, supreme court yenye itaangalia habari ya Katiba, tunasema nani anaweza kuwa judge, mahakimu, nani mwenye hawezi kuwa, na ni kwa sababu gani nao pia kuitimu imewapatia maneno ya kuitimu lakini tumesema hiyo haitoshi, lazima awe ni mtu mwenye hana nini? Awe hana nidhamu ndio akuwe hakimu? Ni lazima ni mtu mwenye hana hufisadi. Niliangalia sijui kwenye gazeti niliona kuna haja gani, why hire a lawyer when you can buy a judge. Ati kuna haja gani kumuajiri wakili ikiwa unaweza kumnunua akimu. Sasa tunataka uhakimu wenye hanunuliki, wenye dhamana wenye hanunuliki, ndio

tumeleta mambo mengi sana juu ya koRti, tumeweka court ya supreme, tumependekeza court zingine, tumezipa nguvu nyingi na pia tumeweka orodha ya vile mahakimu watakavyo ajiriwa.

Kwa hivyo ndio tumesema ingawa mwishowe Rais atamchagua hakimu lakini atakuwa amekubalika na Judicial Committee ya Tume ya kuajiri mahakimu, na hii Tume itakuwa na watu wengine wenye ni mawakili. Kutakuwa na chama cha mawakili na itakuwa pia na watu wa kaniza na watu wengine. Ndio iweza kusema hayo majina ya mahakimu kumi, yeyote anaweza kujaguliwa kutoka kwa hawa. Ikawa wapelekwe Bunge na ikikubali fulani, na sio Rais anateua.

Tumepatia waislam court ya rufani, walikuwa hawana, wana koti moja pekee yake na pia ningetaka kueleza hii ni kuwa, koti ya waislam, ya kadhi, inawajibu wa kufanya kezi za ubinauzi pekee yakee juu ya mtu kuolewa, kuoa, kurithi, hizo ndizo sheria za islam court. Hiyo tu ndio inatekelezwa kwa koti ya kadhi ya kislam. Mtu akiwa ameiba, ameibia nani, ikiwa umeiba wewe, umekosea mtu, kwa hivyo hiyo kezi haiwezi kwenda kwa kadhi, ni lazima hiyo iende kwa koti ya kawaida. Ndio kwani mtu akikuibia wewe ukienda kwa koti unaenda kama nani? Unaenda kama? Umeshashitaki kwa police, siku yenye unaitwa kotini unaitwa kama nani?

**Audience:** Witness.

**Com. Salome Muigai**: Unaitwa kama witness, siyo mlalamishi tena. Wewe ni mshaidi wa kazi, wewe ni shaidi wa taifa……………….***(inaudible).*** huyu mwenye kuiba amekosea nani?

**Audience:** Taifa.

**Com. Salome Muigai**: Kwa hivyo ni vizuri kuelewa tofauti ya hizo. Na hiyo kesi haiwezi kupelekwa kwa Kadhi, hiyo inapelekwa kwa koti ya Taifa.

Twende kwa sura ya kumi, hapa na ni vilee mlitueleza kuwa kuwa Serikali ya Nairobi iko mabli sana nanyi, saa ingine inataka kukata tikiti ya kwenda kuchukua title deed ya shamba moja, lazima uende na nyingine, ndio upate nauli, si ni ukweli?…….sasa ndio haya mambo yote yenye inatwambia kwenye sura ya kumi, ni ya kujaribu kuleta serikali Karibu na watu. Kwa hivyo, tutakuwa na serikali katika kijiji, kutakuwa na serikali katika kata, wilaya. Na mikoani, kazi ya Serikali yensye itakuwa mikoani ni ya ku- coordinate. Ku-coordinate ni kufanya nini? Ni ya kuwakilisha na kuunganisha. For example tukiwa mkoa kama Rift Valley haijapatilishwa, watu wa Trans Nzioa wakiwa hawana store za kuweka mahindi vile wa livyo na mahindi mengi, na watu wa Kajiado hawana mahindi, sasa ni kazi ya Serikali ya mikoa kutafutia watu wa Transnzioa soko ya Kajiado. …nao watu wa Kajiado wana wanyama wengi na mifugo pia wanaweza kuwaleta hao mifuko. Kwa hivyo, kazi yao ni ku-coordinate, ni kushikirisha na kuwakilisha na kushikanisha. Lakini mambo yale ya muhimu ya itakuwa wapi?

**Audience**: Wilaya.

**Com. Salome Muigai:** Wilayani, mambo yale muhimu yote yatakuwa wilayani. Hebu tuangalie sasa sura ya kumi na moja, ninafanya haraka kwa ajili ya mvua. Hii sura imezungumzai habari ya ardhi ama mashamba, na mali. Tofauti ile kubwa iliyoko katika ya Katiba iliyoko hapa na Katiba yenye tunaleta ni kusema kuwa ardhi imerudishiwa watu, tunasema arithi ni ya watu wa Kenya. Kama hawa watu wawe ni mtu binafsi ama jamii ama taifa nzima. Kwa hivyo, sasa mali ya arithi siyo ya serikali tena. Zamani tulikuwa tukisema arithi ni ya serikali ama ardhi ni state. Sasa tumesema aridhi ni ya watu, kwa hivyo watu watafikiria vile watafanya na ardhi yao.

Kitu kingine ningetaka kuwaeleza ni kuwa, shida za mashamba tulielezwa nyingi, nyingi sana, na tukaona itajukua mda mkubwa sana tukisema tutazitatua. Kile tumetaja sasa ni kuweka kikao cha Katiba chenye kushughulikia habari ya mashamba. Lakini, tofauti ya hiki kikao na vile vingine ni nini? Ni kuwa kila mara pili kwa mwaka, kitaenda kwa Bunge kueleza kimefanya nini, kimefika wapi, kina shida gani. Na kwenda kuambia Bunge na Bunge tumekubali itanazwa moja kwa moja na radio na runinga za television na nyinyi mtasikilizwa wapi? Hapo, wananchi watasikia na pia wakubwa wetu watueleza na kuleta shida silizoko kwa upande wao.

Na pia mambo ya ardhi inafuatana sana na mambo ya mazingira, tafadhali mngezongea. Mna mkutano mwingine pale na tulikana tuna mkutano mmoja leo? Mna mkutano mwingine pale nyuma? Habari ya ardhi nimesema hatutaongea zadi, mtasoma chenye kiko lakini tujue kuna Tume yenye itaendela na hiyo kazi. Ni kweli hii Tume ya Njonjo bado inaendelea na haijatupa maoni yake vile walivyoona. Lakini sasa itawakilisha na hii Tume nyingine yenye tulileta na hii Tume nyingine italeta maneno kwa Bunge na siyo kwa mtu yeyote. Lakini Bunge ikiletewa tulisema Taifa linafanya nini? Lina letewa habari moja kwa moja.

Ningetaka kueleza kidogo juu ya sura ya kumi na mbili, inawaelezea habari ya mazingira. Na neno moja tu nitakalo sema habari ya mazingira, tumesema kila mwananchi mwenye kufikiria mazingira yana nyanyazwa anaweza kwenda kwa mahakama akasema nini, tumewapa wananchi haki ya kwenda kwa mahakama kuzuia na kulinda mazingira yetu.

Sura ya kumi na tatu inazungumzia habari ya pesa za umaa na mapato ya uma. Hiyo ina mambo mengi. Pia utosaji wa ushuru na lengo gani ushuru utakapoitishwa na nani mwenye atapatiana ruhusa ya kutumia pesa za uma. Lakini kuna jambo moja tu ningetaka kuwaeleza juu ya hiyo, tumesema, ushuru utalinganishwa na huduma. Hi habari ya kuwa wananchi wanalipa ushuru lakini hawajui inafanya nini, Katiba inakanisha, inasema wanachi wakikuchagua na mission, kutakuwa na nini? Na huziano kati ya ushuru wenye wananchi wanaitishwa na huduma zenye wanapatiwa. Kwa hivyo kukiwa wakati mwingine hawapati huduma, na wasilipe nini? Ushuru.

Sura ya kumi na nine inasema habari ya Public Administration, kulikuwa na ulalamishi mwingi kuhusu huduma za uma, Polisi, Prisons, kwa hivyo tafadhali mkisoma hapo mtaona mambo fulani yenye tumetilia maanani. Moja ni ya kusema tumeweka

Tume moja, office nyingine ya mtu mwenye anaitwa kulinda wananchi, the public protector. Mtu huyu kazi yake itakuwa kufanya nini? Kulinda wananchi, kwa hivyo wewe ukisikia kuna mtu mwenye hajakutumikia vyema, na ni mfanyi kazi wa Serikali,yaani ni Serikali ya umaa kwa hivyo ni mwahajiri wa nani? Ameajiriwa na nani?

**Audience;** Na sisi

**Com. Salome Muigai**: Na nyinyi huna nafasi ya kwenda kulalamika na huyu kazi yake ni kusikiza vile umesema na kufuata na kuona kuwa umepata haki zako.

Sura ya kumi na tano ni juu ya Defence and National security, hao ni nani? Majeshi yetu, police hayuko kwenye majeshi na pia tumewawekea kuwa na the Kenya Police service sababu gani? Kila bahali penye tumeenda tumeambiwa vile police wanaajiri watu, wanawafanya watoto wetu kukimbia na kuhema na kutoa shati lakini hatuoni hawa watu wakiajiriwa. Kwa hivyo sasa tumeiba Tume ya waajirishaji wa Police wenye wataeleza wakuje police wangapi, kutoka wapi, wangapi wametoka pahali fulani, na tunatoa police wetu wapi?

Sasa tulisema kuwa sura ya kumi na sita inausisha habari ya leadership and integrity. Yaani tulisema viongozi wetu hatutahiji wakuwe wasome pekee yake lakini tutahitaji pia wakuwe na nidhamu fulani. Kwanza tumeweka Tume ya kuchunguza mimi Salome Wairimu Muigai nikitaka kusimama Cherangani, Kwanza nitaoneshana makaratasi yangu vile nimesoma lakini mwishowe nitaenda kwenye hii Tume ili ieleze kuwa nidhamu yangu inakubalika ama la……integrity Commission yenye tulianzisha.

Sura ya kumi ni Commission zenye simeanzishwa, kwa nini tumeanzisha Commissions fulani, tumeanzisha Tume fulani kwani saa ingine kuna mengi yenye tunataka ya yafanywe na tunaambiwa yatafanywa, hakuna yule mtu mwenye tumepatia hiyo jukumu ya kuifanya. Kwa hivyo tumeanzisha Tume fulani zenya sitakuwa sikiuliza mambo yamefika wapi na mko wapi, mnatazamia kufanya vipi hili, mnasikia? Kwa hivyo hatutaki kuwambia tutafanya hii mambo kwenye tutakapo patikana, tunataka kuambiwa kuna pesa, na itatuwezasha kufanya kitu fulani na kufikia mwezi wa kumi mwaka ujao tutakuwa tumefika pahali fulani. Tume yenye tumesema nani mwenye atakuwa akituhuzisha kwenye hizi Tume nani ataweza kuchaguliwa kuingia kwenye hizi tume, atachakuliwa na nani, ataondolewa aje ofisini, hizi tume zitatoa wapi pesa ya kuwakubalisha kufanya kazi zao, na wapatiana report za namna gani. Tume zingine zitapatiana report mara moja kwa mwaka, Tume zingine mara mbili kwa mwaka, Tume zingine sitauziana kazi gani yenye inafanywa, ndio ijulikane report zake ni mara ngapi.

Kuna tume kwanza ingine mpya ya kuangalia mishahara ya uma, ya kila mtu, kutoka kwa Rais mpka kwa mtu wa njini kabisa kwenye kazi ya uma, ili watu wengine wasipate shilingi milion mia tano na wengine pate mia tano na nao wote wakienda kukunua majani, wanausiwa bei ngapi?

**Audience**: Bei moja.

**Com. Salome Muigai**: Bei moja. Pia tumepata tumeweka Tume ingine ya Katiba, na hii Tume tumeiba mhula moja pekee yake wa miaka tano. Kufikia miaka tano wawe wamemaliza kundeleza hii Katiba na kuwasiliana na Bunge kuona sheria zote zetu zimeambatana na nini? Na Katiba. Baada ya miaka tano imalizike, waende wakafanye kazi zenye walikuwa wakifanya mbeleni. Kuna Tume ingine moja yenye nilikuwa nimeizungumzia ya haki za binadamu, hii ni Tume ya malalamishi, lakini yenyewe pia itatoka nje iangalie haki za binadamu zina zinatunzwa namna gani. Kwenye hii Tume kutakuwa na watu hata mtu mwenye kazi yake ni kulinda haki za watoto, Watoto wetu haki zao zinalindwa namna gani na wale watu wengine, kwa hivyo kazi yao kubwa ni kuangalia na kutekeza matakwa ya sura ya tano. Ile ya haki za binadamu. Imezungumzia ethics and intergrity, ya Tume ya ethics na intergrity, yaani ni Tume ya kuangalia tabia za watu, na miniendo ya watu kabla hawajakuwa viongozi na pia wakiwa viongozi uongozini. Kiongozi wetu ikiwa tabia zake haturidhishi, hiyo ndiyo Tume yenye tutapelekea malalamiko yetu.

Chapter eighteen, amendment of the Constitution, ama sura ya kumi na nane inangalia vile Constituion ama Katiba hii yetu inaweza kubadilishwa. Tena kuna kile kipengele chenye kitakubalisha pengine Bunge kubadilisha, na tunasema kitabadilsha kwa wingi wa watu. Lakini pia tunasema kuna parts zigine wakitaka kubadilisha lazima waturudie sisi wananchi na tuwape za maoni ndio waweze kubadilisha.

Sura ya kumi na tisa ni ya habari ya kutafsiri haya mambo yote na sura ya ishirini ya mambo yenye tumewekea maanani ya kutuwezesha kutoka kwa kwa Katiba moja mpaka kwa nyingine. Kwani hatutaki pengo. Kwa hivyo tukiwa tunasema hii lazima mpaka ifanywe kwa katiba mpya, kwa mfano, tumesema tunataka Tume ya uchaguzi ya watu kumi. Lakini wakati huu tuna watu wangapi? Ishirini na zaidi, kwa hivyo tumesema, uchaguzi wa kwanza unafanywa na hao wenye Tume wenye wako, wakimaliza, tutawapa siku tisaini wamalize, hiyo ni miezi ngapi? Miezi tatu, wamalizie habari ya uchaguzi huo wote na wakati huo pia mtakuwa mkileta wale wengine wenye tunataka, tutakuwa tukileta wale watu wengine wenye tunataka, tutakuwa tukileta Tume mpya. Hatusemi mwenye alikuwa kwa Tume ………

Halafu mwishowe ni hile mijadala yenye imekuja, the schedules, ni kuoneshana mavieti tukijua sisi ni wakenya, nchi yetu inafika wapi na pia ile viapo vyenye tukiuliza viongozi wetu kuchukua ndio watuongoze na mambo kama hayo. Hata hiyo pia mtasoma mkiwa nyumbani. Kitu kimoja ningetaka kusema kabla sijamazia ni pia kwenye hii Katiba mpya ni mwananchi ana haki ya kumrudisha kiongozi nyumbani kama hajafuraishwa naye, ukipeleka mbuge, baada ya miaka miwili akuwe hamumuoni, hafanyi lolote lenye mlimtuma, mnaweza kumrudisha nyumbani. Kwa hayo mengi sana, Asanteni sana.

**Emannuel Satia:** Asante sana, tunahakika kwamba hata leo pia tumeleta baraka, kwa sababu mvua imenyesha hivi. Sasa tutachukua hatua ya pili. Zamu yetu inahusisha mambo hayo, kwa sababu tumekuwa tukizunguza hii Katiba mapendekezo mnasema nini. Basi kuna mahali ambapo unafikiria, una swali ama ungetaka maelezo zaidi. Sasa tutakupa nafasi ya kuuliza, hata

ukita maelezo kidogo. Katika zile list kuna watu ambao wakuwa wamejiandikisha, lakini kuna wengine walikuwa wamefika mapema na hawakuwa wamejiandisha, kwa hivyo list hizi tutapeana wale ambao walikuwa hawajiandisha. Tungalipenda tujue watu wamgapi waliofika katika mkutano wetu wa leo. Mara nyingi Commissioner alikuwa akiniambia kwamba, mahali pote alipoenda Kenya Nzima Eldoret ikilikuwa na watu wengi wengi sana katika mkutano wao. Na sisi tungependelea jambo hilo. Asante.

Tutachukua maswali kutoka kwenu, tunachukua maswali kumi kisha tujaribu kuwajibu halafu nijukue zingine kumi na pia tujaribu kuwajibu. Kwa hivyo hebu tuache kelele kidogo ili tumalize mkutano huu mmoja tulivyo kubaliana. Sasa tutachukua maswali kumi tuwajibu kisha tuchukue mingine kumi. Na tungependa ikiwa, ukipata swali ambalo limeulizwa usilirudie. Na pia ukipewa nafasi ya kuuliza swali, tungelipenda uulize swali bila kutoa maelezo mengi, uliza swali tu njizi unavyotaka ifahamishwe zaidi, sawa sawa.

Akina nani tunaweza…………mimi ningalipenda kwanza, tukijakuana tuanze kwa kuseme moja pili tatu mpaka kunu, ili kila mtu apate nafasi. Msipendelee wazee sana na wakina mama mkutano imeleta ubaguzi la, ni njia moja ya kuwashirikisha ya kuakikisha kwamba kila mtu anapata nafasi,ya kuuliza maswali. Katika kikao hiki mimi nitakuwa mwenye kiti. Commissioner atajibu maswali tu, kwa hivyo ukijukua mda mrefu nakwambia tafadhali wajia pale. Lakini sasa tualize maswali kwa njia gani? Tuanzie wale watu wa nmyuma kwa line ya kwanza, tutaanzia nyuma mpaka katikati pale, tuchukue watu kumi kutoka nyuma, kisha kwenye line ya pili, tutajukua watatu wengine halafu tena itakuwa mwisho. Sasa hebu tuchague watu kumi wa kwanza. Kuna msichana hapa ashaketi, ndio yeye mtu wa kwanza, kama kuna watu wengi mtu wa pili, mzee huyu wetu atakuwa wa tatu, yule kijana atakuwa wa nne, wewe utakuwa wa tano, yule atakuwa wa sita, wa saba yule, wa nane, yule atakuwa wa tisa, yule mzee wa pale katikati atakuwa wa kumi.

Baada ya kuuliza ya maswali tungelipenda tu tujue habari kuhusu, jina lako ni nani, anwani yako, na pia utatuwekea kule chini. Kwa upitie kule kando ili mje huku, wa kwanza kuuliza maswali aulize kisha kuna hii register katika meza atafaa kujukua habari kukuhusu. Jina, anwani, na wote karibu. Kwa hivyo tuanze na yule mtu wa kwanza, l think itakuwa vyema ili iwe rahisi.

Twambie majina kisha uhulize swali swali.

**Dismas Momanyi**: Wananchi wenzangu hamjamboni, kwa majina ni Dismas Momanyi, kutoka Kabtarot. Swali langu ni hili, kuna mahali kwa mjadala wetu tumesikia ya kwamba tuna uhuru wa kuabudu, sasa ninashindwa kuelewa ni kuadudu katika hali ya kusikiza Mungu ama ni kumwabudu Shetani, kwa maana katika Kenya kuna badhi ya wale ambao wanamwabudu shetani. Kwa hivyo ningependa kuelezewa kwa kinaka upaga, tuabudu Mungu wa aina agani. Swali langu ni hilo?

**Emmanuel Satia:** Asante sana. Mtu wa pili.

**Philemon Birget**: Kwa majina ni Philomon Birget, ninatoka Milimani. Swali langu ni kwamba, katika Constitution nilisikia kwamba wanasema labda wamesaidia madaraka fulani fulani na ikiwa kama Prime Minister anachaguliwa kama kwa Parliament, je hiyo Constitution itafunjwa ili apewe yule mtu mwenye alikuwa anaingia ama namna gani?

**Emmanuel Satia**: Halafu pale, watatu.

**Julius Kanazo:** Jina langu ni Julius Kanazo, ni kuhusu uhuru wa kuabudu Mungu, katika uhuru wa kuabudu bia kuna uhuru wa…………………….***(inaudible)*** kuwe nanyo, kwa mfano vijana …………………………***(inaudible)*** vijana wamechochewa, na kuna ile tabia na vile, saa ingine wengine hauwezi kujua vile wanamendelea. (inudible.)

**Emanuel Satia**: Asante sana yule wa tatu.

**Julius Luyo**: Kwa majina ni Julius Luyo. Sana sana ile mbaya serikali yetu ya Kenya kama mtu alishikwa, ama afisa wa Serikali ameumiza mtu fulani, labda alikuwa na makosa ama hakukuwa na makosa, halafu unakuta amepekwa kule ndani korokoroni,……kisha wameongea na yeye kuhusu kisa chake pamoja mwenye na ameumiza mwingine, halafu unakuta, mtu amepita kando na kitu kidogo, lugha yao hao police, wanasema ni kitu kibwa, amepewa, halafu yule aliyeumia,…………. ***(inaudible)*** kama aliumia sana, baadaye unakuta huyu hakimu, amesahau hiyo maneno, sasa swali ni hili, watu kama hao mahakimu ni mzuri waelewe hiyo kazi ama wafutwe kazi?

**Emmanuel Satia**: Ningalipenda uhulise maswali kuhusiana mjadala tuliyokuwa nao. Asante.

**Daris Busamania**: Swali la kwanza, tangu zamani, zama za kale, swali la kwanza ni hili, katika draft je, tumewacha wapi developing na ………… …mlituelezea mkasema kwamba hakutakuwa na forced labour, na je wakubwa ile kazi wanafanya ni ya kuwakilisha ama hapana. Kwa mfano ukiwa korokoroni hapa, wanakwambia ………….wengine mnasaidia kutusaidia hapo ndani.

Na makasema kwamba kutakuwa na Bunge la wilaya na pia tangu zamani tumekuwa na wabunge ile nyingine ya local Government, hao watakuwa wapi? They are working somewhere, hayo watakuwa wapi?…………….

Mlisema waziri hatakuwa MP tena, na je President atakuwa wapi? Upande wa polisi, mlisema mngependa wajiandikishe na kutoa report kutoka kila sehemu ni wanagapi wanachaguliwa kutoka katika kila Kabila. Na tungependa kila department pia iondoe hiyo number kwa sababu kama armed forces, kuna kabila fulani lina watu wengi saidi, kabila zingine sina mtu moja. Halafu pia kutakuwa na mjadala wa radio, tuwe tukizia mijadala ya Bunge iwe ikutufikia kutoka kwa radio live..

**Emmanuel Satia**: A sante sana una maswali mengi mazuri, haya hebu tupatie majina tafadhali.

**Arap Too:** Mabibi na mabwana hamjambo wote, jina langu ni Arap Too na nina kuja kutaka hapa……, niko na maswali manne, niko na maswali manne, swali la kwanza linaenda hivi, katika sura ya sita juu ya mahakama, na mambo ya shuria, sasa juzi tulikuwa ama tuliweza kuona njizi tunasema ya kwamba wale majudge ama wale mayors walisoma, walisomea majudge mengine waninne, hasa ningependa kuhuliza kuwa ni hivi, ni sehemu ambayo hawakutaka ijaribiwe, hata na sisi tuweze kuelewa ni kitu gani wanataka kupita, kwa sababu hata halama hizi zote sisi………..lakini nitaka mieleze kinaga ubaga ni sehemu gani hawakupendelea.

Swali la pili linatoka katika sura ya kumi na tano (A) elfu kumi na ninety, tumeambiwa kwamba jambo la kwanza tunatakiwa tuelewe sheria ama Katiba. Lakini mpaka wakati huu, baada ya miaka karibu arubaini sasa, hatujawai kuona Katiba ya Kenya, tukiwa nayo ama watu wengi namna hii waweze nayo katika maktaba yao. Sasa hii Katiba mpya tutapata namna gani ili tuweze kuelewa yale yote ambayo sisi tumeweka ndani na tumekubaliana hivi turudi kufuata. Kwa sababu hatuwezi kufuata mjadala ambao hatuelewi.

Haya la tatu, kuna district Government katika sura ya kumi. Kwa kweli kutoka huko nyuma, kuna serikali ya kijiji, serekali ya kata, kuna watu ambao ni wachache, na hao watu wanaweza kushiriki katika kuunda Serikali ile ndogo, lakini ikifikisha Serikali ya wilaya, kwa sababu ni wachache hawatapata yule mtu mwenye anaitwa representative wao. Kwa hivyo hawa wamekuwa wamepuuzwa, sasa mambo yao yalindwa kwa njia gani? Hawana muwakilishi wao huko juu?

La mwisho, ni minority seats, kuna minority seats kati ya viti tisaini, ningependa tuelezwe namna hawa ambao wamejaguliwa tuseme katika eneo hili la ubunge , tuseme kuwa namna gani ama ni kwa njia gani tunaweza kupata watu hawa..

**Emmanuel Satia:** Asante sana Bwana Too maswali mazuri sana. Tafadhali mzee karibu, sima majina kisha uluze maswali.

**Dr. Waweru Wambugu:** Thank you madam Chairman, my name is Dr. Nicholas Waweru Wambugu, I am a retired Kenyan servant.hamjamboni?

**Audience:** Hatujambo.

**Dr. Waweru Wabungu:** I will try to speak in English because my Swahili is broken. I did common health in 1952…………………………………………………………***(inaudible)*** by the British Government. Then from there l was given a certificate 1961, and the legislature was(Inudible)……………………………………………………………………………… we have a problem of education, unemployment and they wasy I have seen in this constituion……
…………………………………………………………………………………***(Inaudible).***

**Emmanuel Satia**: Asante sana, asante Daktari, wale wawili wa mwisho halafu tupate majibu. Tupatie majina halafu uendelee.

**Wanjala Charles**: Hamjambo wananchi wenzangu, mimi ni wajala Charles swali langu ni fupi sana, the bill of rights chapter five. Kuhusu haki za watoto,…………kuna section inayosema lets burn corporal purnishment, ningependa kujua tu njizi tutakavyo tekeleza sheria hiyo bila kudhuru jamii zetu, kwa sababu tayari kama walimu tumejaribu na tumeshindwa, sasa tunashindwa ni vipi corporal purnishment itakosa kutekelezwa bila kwanza kuanzia kule nyumbani. Na ile section tungependa Commissioner atueleze any scientific evidence ya kuonyesha ya kwamba yule mtoto wa wazamani alikuwa tofauti na yule wa sasa. Asante.

**Emmanuel Satia:** Asante sana ni mwalimu kweli mwenyewe. Mtu wa mwisho utupatie jina kisha aulize maswali.

**Barnabas Kibitichi:** Mimi ni Barnabas Kibitich kutoka Elbargon na ningetaka kuuliza kuwa katika sehemu ya ukulima njizi bei ya bidha zao ili wakulima waweze kulindwa zaidi katika kupewa faida ambazo zinapatikana kutoka kwa mazao yao wasije wakauza kwenye bei ya hara ambayo itawafanya wakulima wakuwe na mafuta ya kuendesha kazi zao na ili waweze kuendesha Kilimo chao. Katika kikao hiki nimesikia kuna wabunge wa wazira kama mbuga, kilimo, nafikiri kutahitajika kuwe na elimination kutoka kwa wakulima pia, katika zile instituion ambayo itashida haki ya wakulima wote na usafirishaji wa vyakula ama mifugo kutoka sehemu zingine hati zingine.

Swali ni hili wakati wa uchaguzi huo wa wabunge hawa, tunahitaji pia Commission ijue ya kwamba tutahitaji tupewe mpinu za kuweza kuwasiliana na wabunge.wetu wakiwa sehemu mbali mbali.

**Emmanuel Satia:** Sasa nitampa nafasi Commissioner ili atusaidie. Karibu Commissioner.

**Com. Salome Muigai:** Asante sana Bwana mwenye kiti, haya maswali nitajaribu kuyajibu vile niwezavyo. Lakini mengi yao yanakuja kwa sababu watu hawajaisoma haya maandishi ya Katiba mpya. Mengine tayari nimeshaakilishwa kwenye haya maandishi na ningeomba tafadhali, myasome ndio muone pahali pana pengo na kama ukisoma ukikuta bado kuna pembe tafadhali utaandika matakwa yako na upendekeze wakati wa kutulea halafu mpee bwana coordinator atatuletea.

Sasa Mwanzo Dismas anataka kujua ya kwamba hii hii free of worship ni kama ni haki ya kuabudu Mungu kuwa lazima tusome kwa Katiba kuwa kuna uhuru wa kuabudu Mungu. Lakini nikisema hiyo Katiba Sheria nayo ina kikomo chake. Ukisoma ni lazima uabudu Mungu ni lazima utafsiri maana yake Mungu ni nini na maana yake Shetani ni nini. Hiyo ilitutatiza zaidi na tukajua tutasema Mungu, how to you relate to God. Tutasema Mungu ni nani? Mwenye ninasema aabudiwe, kama kuna haki ya kuabudu, Mkikuyu akitaka kuabudu Mungu wake mwenye anaka Mt. Kenya, amefunja sheria? Dini ya mazambwa akitaka kuabudu Mungu wake mwenye kukaa Mt. Elgon, amefunja sheria? au Mungu wa …….. Mungu wa Kirsto wa ………… na wengine wetu sisi, na yule Mungu wa Allah wa Muslims, na yule wa Hindu. Kwa hivyo wakati wa kuja kuzungumzia habari

kusema ni double sytem, ilitupa shida sana. Tusema basi lakini na kwingine pia, nani mwenye anaweza kukata kanisa lenye kumuomba Shetani, kusema maybe yule Mkikuyu ni Mungu wangu, kwa hivyo kama waselima tuabudu Mungu, huyu ndiye Mungu wangu.

